**USAILI** ajira mpya walimu Januari 14
UKURASA 2

**TRA** yavuka lengo yakusanya Tril. 3.5/-
UKURASA 5

**BMH** kupandikiza figo kisasa kwa roboti
UKURASA 8



**ARTETA: ARSENAL HAIPOI MBIO ZA EPL**
UKURASA 22

epaper.ippmedia.com
Nipashe
MIAKA 30
Nipashe
Mwanga wa Jamii
www.ippmedia.com

Alhamisi Januari 2, 2025 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
ISSN 0856 • Na. 0581910
epaper.ippmedia.com

LIKE & FOLLOW US 0677 020701 nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ The nipashe Digital nipashedigital

# Lissu ataja mambo 7 kuufanya uchaguzi CHADEMA kuwa huru

UKURASA 2



Tundu Lissu

# Othman ajitosa urais Z'bar

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ametangaza rasmi ataomba ridhaa ya Chama cha ACT-Wazalendo kumteua kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Sambamba na hilo, Othman ameweka wazi kuwa vyovyote itakavyokuwa, hata bila Katiba Mpya, ACT - Wazalendo itashiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Alisema hayo jana

ENDELEA UK. 3



Waumini wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Mlandege mkoani Iringa wakiupokea mwaka 2025 kwa maombi ya kuliombea Taifa jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

UKURASA WA 24

## FADLU: TUTAPAMBANA UWANJANI DAKIKA ZOTE

WAKATI kikosi cha Simba kikitua salama nchini Tunisia tayari kwa mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho hatua ya makundi dhidi ya CS Sfaxien, Kocha...

## Viongozi wa dini watoa angalizo Uchaguzi Mkuu, amani, kutenda haki

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA YAIFUATA SIMBA KWA RUPIA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akiwa na waumini mbalimbali katika maandamano ya kuingia kanisani wakati wa ibada ya Adhimisho la Misa Takatifu ya Sherehe ya Bikira Maria Mama wa Mungu na Mwaka Mpya 2025 iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# Lissu ataja mambo 7 kuufanya uchaguzi CHADEMA kuwa huru

**Na Jenifer Gilla**

JOTO la uchaguzi wa nafasi ya uenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) likiongezeka, mgombea wa nafasi hiyo, Tundu Lissu amependekeza mambo saba yanayopaswa kufanyika ili uchaguzi huo uwe huru na haki.

Baadhi ya mapendekezo hayo ni kualikwa viongozi wa dini, mabalozi kutoka nchi jirani ambao watakuwa waangalizi pamoja na kura kuhesabiwa mchana.

Amesema mapendekezo hayo yakifanyika ipasavyo yatasaidia kuondoa mianya ya rushwa, kudhibiti watu wenye nia ovu ya kuvuruga uchaguzi.

Aliyasema hayo jana wakati akitoa salamu za mwaka mpya 2025 kwa wanachama wa chama hicho na Watanzania.

Ameunga mkono hoja ya kuwa na uchaguzi huru na wa haki ndani ya chama, kinyume na hapo hakitoweza kutekeleza kivitendo matakwa ya kikatiba ya kutengeneza uongozi unaoweza kumilikiwa, kuhojiwa na kumilikishwa na umma.

**VIONGOZI WA DINI, MABALOZI**

Alisema ili uchaguzi huo uwe huru na wa haki, alipendekeza Kamati Kuu ya chama iwaalike viongozi wa dini kama wageni waalikwa na watazamaji ili kuzuia watu waovu kuvuruga uchaguzi huo.

Alisema amependekeza suala hilo kwa sababu chama hicho kina upungufu wa wazee wastaafu ambao katiba inaelekeza wachaguliwe na kamati za chama kwa ajili ya kusimamia uchaguzi huo.

Pia, alishauri Kamati Kuu kuwaalika mabalozi wa nchi jirani ambao ni rafiki ili kuongeza uzito wa uchaguzi na kuongeza macho dhidi ya waliopanga kuharibu uchaguzi huo.

**MATUMIZI YA FEDHA**

Alitaja pendekezo lingine kuwa ni kamati ya wazee wastaafu wa chama kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Mkuu kuhakikisha kuwa fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya usafiri wa wajumbe wa vikao vya uchaguzi zitumike kukodisha mabasi au usafiri mwingine utakaowasafirisha kutoka maeneo yao hadi Dar es Salaam na kuwarudisha.

Alipendekeza fedha zilizotengwa kwa ajili ya malazi ya wajumbe zitumike kukodi nyumba za kulaza wageni watakazotumia katika kipindi chote watakapohudhuria vikao vya uchaguzi.

Alisema na fedha za chakula na mambo mengine zilipwe kwa wajumbe watakapowasili jijini.

Kadhalika, alisema mwaka 2012 chama hicho kilitengeneza miongozo ya uchaguzi ambayo pamoja na mambo mengine inazuia utoaji wa rushwa katika uchaguzi, ikiwamo kutoa fedha, chakula, zawadi, au rushwa ya ngono kwa wajumbe au wapigakura kwa lengo la kujipatia fedha.

Aliwasihi wajumbe wa timu yake ya kampeni, vongozi wa wanachama na wafuasi wake kuchukua tahadhari kulinda maisha na usalama wao na kuepuka vishawishi vya kuwa chanzo cha vurugu.

**KURA KUHESABIWA MCHANA**

Alipendekeza Kamati ya Wazee Wastaafu watakaoteuliwa kusimamia uchaguzi kuhakikisha kuwa kura zinahesabiwa mchana ili kuepuka watu wenye nia mbaya kutumia giza kuleta vurugu na kuharibu uchaguzi.

> **Ameunga mkono hoja ya kuwa na uchaguzi huru na wa haki ndani ya chama, kinyume na hapo hakitoweza kutekeleza kivitendo matakwa ya kikatiba ya kutengeneza uongozi unaoweza kumilikiwa... kuhojiwa na**

**KUTANGAZA MATOKEO**

Alipendekeza shughuli yote ya kupiga na kuhesabu kura na kutangaza matokeo ya uchaguzi ifanyike kwa uwazi mbele ya wajumbe wa mkutano ili kuondoa uwezekano wa kuingiza kura haramu au kubadili matokeo.

**WAPIGAKURA**

Alishauri watakaoruhusiwa kuingia katika mkutano ni wajumbe, waalikwa na wahudumu maalumu wenye vitambulisho na wagombea au mawakala wao wanashirikishwa katika hatua zote za maandalizi ya mkutano.

Pamoja na mambo mengine, Lissu alishangazwa na mapokeo tofauti ya baadhi ya viongozi wa juu wa chama hicho kuhusu mapendekezo ya ukomo wa madaraka, akisema linaloonyesha kuwa wana lengo la kuirudisha nchi nyuma kikatiba kwa zaidi ya miaka 40.

Aidha, anashangazwa na maoni ya baadhi ya viongozi hao kuwa hoja ya ukomo wa madaraka haifai kutekelezwa ndani ya vyama vya siasa hasa vya upinzani kwa sababu uongozi wake hauna malipo.

"Hoja hii inapaswa kuangaliwa kwa tahadhari kubwa, kama lengo la ukomo wa madaraka ni kudhibiti ving'ang'anizi wa madaraka na kuhakikisha utaratibu wa kuachiana madaraka kwa njia za kikatiba, ukomo wa madaraka unawahusu viongozi wote wa kisiasa bila kujali wanajitolea au wanalipwa mishahara," alisema.

Alisema tangu nchi iingie kwenye mfumo wa vyama vingi, ni viongozi wa vyama vya upinzani pekee ndiyo wameng'ang'ania madarakani kwa muda mrefu zaidi jambo linalowatia doa katika harakati zao za kudai mfumo bora wa kidemokrasia katika uchaguzi na utawala wa nchi.

Alisema hali hiyo pia imesababisha nafasi za uwakilishi wa viti maalumu katika ubunge na udiwani kuwa za watu wachache, wanaojijengea himaya za kimalkia ndani ya vyama vyao kwa kutumia mafao yao kuendelea kubaki katika nafasi hizo.

Kuhusu Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Lissu alisema unapaswa kutoa mafunzo kwa ajili ya ustawi wa demokrasia, utawala bora na uwajibikaji katika chama hicho (CHADEMA) na taifa kwa ujumla.

"Tutapiga kura huku tukijua kuwa wapigakura feki wataandikishwa, wagombea wao wataenguliwa, vurugu kwenye kampeni na siku ya uchaguzi, kura halali zitaibiwa, kura feki zitaingizwa na wagombea walioshindwa watatangazwa washindi wa uchaguzi hizo," alisema.

Alisema kuanzia sasa msimamo wa CHADEMA unatakiwa kuwa 'bila mabadiliko hakuna uchaguzi' na itawezekana tu kama kukiwa na uongozi mpya, mbinu mpya na fikra mpya za mapambano ya kidemokrasia.

Alisema baada ya miaka 21 madarakani kwa uongozi uliopita katika chama hicho wasidanganyane kuwa miaka mitano ijayo utaleta mambo mapya ambayo hawajayaona.

Lissu alisema mwaka 2024 uligubikwa na matukio ambayo hayakuwa mazuri kwa chama hicho, yakiwamo ya kutekwa, kuteswa na kuuawa kwa viongozi na wanachama wa chama hicho.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*

## Usaili walimu uliositishwa watangazwa tena

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

OFISI ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma imesema usaili wa waombaji wa kada ya ualimu uliositishwa kwa muda utafanyika kuanzia Januari 14 hadi Februari 24, 2025.

Taarifa hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, Lynn Chawala.

Chawala alisema awali ofisi hiyo ilitoa taarifa ya kusitishwa usaili wa walimu Oktoba 17, mwaka jana, kulikotokana na tangazo la kuitwa kwenye usaili la Oktoba 15, 2024.

"Kupitia tangazo hili, Katibu wa Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, anapenda kuwatangazia waombaji kazi wote wa kada za ualimu ambao usaili wao ulisitishwa kwa muda kuwa usaili huo utafanyika kuanzia terehe 14 Januari, 2025 mpaka tarehe 24 Februari, 2025," alisema Chawala.

Alisema wasailiwa wote wa kada za ualimu wanakumbushwa kuwa usaili wa kuandika (mchujo) na mahojiano ya ana kwa ana utafanyika ndani ya mikoa wanayoishi, watapangiwa vituo vya kazi kulingana na ufaulu wao popote nchini.

Aidha, alisema waombaji kazi wa kada za ualimu na walioomba kwa ajili ya kada za amali na biashara wanatakiwa kuhuisha taarifa za makazi ya sasa kwenye mfumo wa 'Ajira Portal' ili waweze kupangiwa kituo cha kufanyiwa usaili jirani na maeneo wanayoishi kwa sasa.

"Tangazo la majina kuonesha mtakapofanyia usaili litatolewa tarehe 6 Januari, 2025 kupitia tovuti ya Sekretarieti ya Ajira, mitandao rasmi ya kijamii ya taasisi na akaunti za waombaji kazi kwenye mfumo wa Ajira Portal," alisisitiza. Vile vile, alisema wote walioitwa kwenye usaili wanatakiwa waende na vyeti vyao halisi vya taaluma, cheti cha kuzaliwa pamoja na kitambulisho halisi kwa ajili ya utambuzi.

Alisema, vitambulisho vinavyotambulika ni pamoja na cha uraia, cha mkazi, mpiga kura, hati ya kusafiria, leseni ya udereva, cha kazi, barua ya utambulisho kutoka ofisi ya serikali ya mtaa au sheha. Alisema Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inawakumbusha watafuta fursa za ajira wote kuwa mchakato wa ajira unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya sifa, haki, usawa na uwazi na wanapaswa kujiepusha kutoa rushwa na kupokea taarifa potofu.

*Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz*



Muuguzi wa wodi ya wazazi katika Hospitali Teule wilayani Muheza mkoani Tanga, Neema Ngoda (kulia), akiwa na baadhi ya wazazi na watoto waliozaliwa katika mkesha wa Mwaka Mpya. Jumla ya watoto sita wamezaliwa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Othman ajitosa urais Zanzibar

**Na Waandishi Wetu,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ametangaza rasmi ataomba ridhaa ya Chama cha ACT-Wazalendo kumteua kuwania nafasi ya urais wa Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Sambamba na hilo, Othman ameweka wazi kuwa vyovyote itakavyokuwa, hata bila Katiba Mpya, ACT - Wazalendo itashiriki Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu.

Alisema hayo jana mjini Unguja alipozungumza na wahariri katika salamu zake za Mwaka Mpya 2025.

"Huu ni mwaka wa uamuzi. Sisi tushiriki uchaguzi. Haijalishi kutakuwa na mazingira gani. Vyovyote atakavyoanguka, ndivyo tutakavyomchinja," alisema.

Alitaja mambo 11 yanayomsukuma kuutaka urais, akisisitiza anaamini yatainusuru Zanzibar kutoka hali ya sasa aliyoita "kuwa nyuma kimaendeleo kulinganishwa na rasilimali ilizonazo".

Mambo hayo ni pamoja na kudai haki na mamlaka ya kuiwezesha Zanzibar kutumia rasilimali zake kujenga ustawi wa uchumi sawa na hata zaidi ya nchi nyingine za visiwa kama vile Mauritius, Seychelles, Cape Verde; kuwarejeshea wananchi haki ya kuwawajibisha wanaoongoza serikali kupitia uchaguzi huru na wa haki na kujenga misingi ya utawala bora unaojikita katika uwazi na uwajibikaji.

Lingine ni kufanya marekebisho ya mfumo wa kikatiba na kisheria ili kuondoa mamlaka aliyoyaita "ya kifalme kwa Rais" kwa kujenga misingi bora ya kuchungana na kutoa fursa zaidi kwa wananchi kushiriki katika uendeshaji wa nchi yao kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo imara na zinazowatumikia watu badala ya kuwa mzigo mwingine kwa raia.

Othman alitaja mambo mengine yaliyomsukuma ni kutaka kujenga umoja wa kweli wa kitaifa utakaoakisi utengamano wa kijamii kwa kuimarisha usawa, haki za raia na mshikamano; kujenga mfumo bora na wenye ufanisi wa kupambana na ufisadi wa aina zote na kuzuia matumizi mabaya ya ofisi za umma na rasilimali pamoja na kujenga misingi bora ya uchumi itayotumia vizuri rasilimali za Zanzibar kwa njia endelevu, ukiwamo utalii wenye tija na unaolinda mazingira na nafasi bora na ya kipekee ya kijiografia ya Zanzibar.

Alisema pia anakusudia kuwajengea wananchi fursa ya kushiriki katika uchumi kwa kulinda haki zao za ardhi na nyenzo za kiuchumi; kuwawezesha wote ambao wamefikia kiwango stahiki cha fani mbalimbali ili wakue na kuzalisha bidhaa na huduma katika soko la ndani na nje; kuwawezesha vijana kuajirika na kujiajiri na kuimarisha huduma za ustawi wa jamii zikiwamo elimu, afya na matunzo ya wasiojiweza na hifadhi ya jamii yenye uendelevu.

Othman ambaye ni Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Taifa, alisema katika kipindi cha zaidi ya miaka 30 cha utumishi wake serikalini, amebaini kiini cha matatizo ya Zanzibar ni uwezo dhaifu wa mfumo wa sasa kiutendaji, sera na usimamizi.

Alisema kuwa kutokana na uzoefu wake huo, hata akashika nafasi ya juu katika taaluma ya sheria - Mwanasheria Mkuu wa Serikali, anaamini anaweza kuivusha Zanzibar kutoka katika dimbwi la matatizo yaliyopo, akisisitiza "inahitaji kunusuriwa haraka".

Alisema ili kuyafanikisha hayo yote, lazima kuwe na utaratibu wa kuhakikisha kuwa kuna uchaguzi huru, wa haki, unaoaminika na wa wazi mwaka huu wa 2025.

Alikosoa mfumo wa sasa wa uchaguzi, akifafanua unakifanya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwa na idadi kubwa ya wabunge na wawakilishi katika vyombo vya uamuzi -- bungeni na Baraza la Wawakilishi ambao "wanapigania zaidi maslahi ya chama chao badala ya maslahi ya taifa."

Alitoa rai kwa viongozi wa serikali na CCM kutafakari kwa kina kinachojiri Zanzibar wakati wa uchaguzi. Wasingependa kuona tena vurugu na hata mauaji yaliyoripotiwa katika uchaguzi uliopita.

Aliendelea kukosoa utendaji usiozingatia maadili serikalini, akirejea Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa Mwaka 2022/23, zote mbili (Zanzibar na Tanzania kwa ujumla) zinabainisha kukosekana nidhamu katika matumizi na usimamizi wa fedha za umma.

Alisema kunaripotiwa hali hiyo ilhali nao ni sehemu ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), lakini wao hawana mamlaka ya kuwawajibisha watendaji wanaokiuka sheria na taratibu zilizowekwa, hivyo wanabaki kuwa jicho la wananchi kama ilivyo kwa CAG.

**UCHAGUZI SIKU MBILI**

Alikosoa Uchaguzi Mkuu kufanyika kwa siku mbili visiwani Zanzibar, akionya kuwa awamu hii hawatokubaliana na utaratibu huo kwa kuwa wamebaini unalenga kufanikisha uporaji ushindi wa vyama vya upinzani.

Pia alisema wanaendelea na mazungumzo na wenzao wa CCM kuhusu hatima ya SUK, akidokeza kuwa wamebaini kukosekana dhamira ya kutekeleza waliyokubaliana wakati wa mazungumzo yaliyofanikisha kuundwa kwa SUK.

"Katika kikao cha mwisho cha Kamati Kuu ni kweli tuliamua tujitoe katika Serikali ya Umoja wa Kitaifa, katika kulizungumzia hili na upande wa pili, zipo ahadi zilitolewa na tunaendelea nazo. Hatujafika mwisho katika mazungumzo haya," alisema.

Othman pia alikosoa Kamati ya Hesabu za Serikali (PAC) ya Baraza la Mawaziri kuongozwa na mwenyekiti asiyetoka upinzani, jambo ambalo ni kinyume cha uendeshaji wa Mabunge ya Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Madola.


Nipashe
WhatsApp Chaneli
Skani hapa kutembelea chaneli yetu


# Viongozi wa dini watoa angalizo Uchaguzi Mkuu, amani

**Na Waandishi Wetu**

WAKATI Watanzania wakisherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya, viongozi wa dini wametumia mkesha kutoa angalizo kuelekea Uchaguzi Mkuu utakaofanyika mwaka huu pamoja na kudumisha amani

Kwa nyakati tofauti viongozi hao pia wamewakumbusha Watanzania mwaka 2025 kutenda haki pamoja na kusaidia wasiojiweza.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Kijitonyama, Dk. Eliona Kimaro, alizitaka mamlaka zinazohusika na uchaguzi mkuu mwaka huu kutenda haki kwa vyama vyote, ili kulinda amani ya nchi.

Akihubiri katika moja ya ibada kanisani hapo, Kimaro, alisema hakutakuwa na muujiza wa amani kama haki haitatendeka kwa vyama vyote vya siasa katika uchaguzi huo.

"Mwakani (2025) tunaenda kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani. Lakini, hamasa tunayohamasisha nchi yetu ni kutenda haki, uchaguzi wa haki ili amani iendelee kuwapo katika nchi yetu," alisema.

Alisema endapo hakutatendeka haki kuna hatari ya kuhatarisha amani ya nchi, ni bora hilo likazingatiwa kwenye uchaguzi huo.

Alisisitiza kuwa amani ni matokeo ya kazi ya nguvu ya haki ambayo haiji bure bali inatafutwa.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Shinyanga, Mhashamu Liberatus Sangu, akihutubia kwenye mkesha wa kuukaribisha mwaka mpya 2025, uliofanyika katika Kanisa Katoliki la Ngokolo Mjini Shinyanga aliwasihi Watanzania kuombea nchi ili iendelee kuwa na amani.

Kadhalika aliwasihi kuwaombea viongozi wenye dhamana ya kuliongoza taifa waweze kuliongoza vyema, bila kusababisha vurugu wala uvunjifu wa amani iliyopo.

Shekhe wa Mkoa wa Mwanza, Hassan Kabeke alisema kwa mwaka huu wa uchaguzi, Tanzania bila kung'angania amani haiwezi 'kutoboa' kwa namna yoyote, ni jukumu la kila Mtanzania kutumia nafasi yake kuidumisha.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Mwanza, Edward Kibiti alisema ni muhimu kuomba ili kupata watu sahihi wa kuliongoza taifa.

Padri George Nzungu wa Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Mwanza, alisema ni wakati wa Watanzania kusimama katika Zaburi ya 127 na kuwa asiyejenga nyumba yake juu ya mwamba huiharibu mwenyewe. Askofu wa Jimbo Katoliki la Moshi, Ludovick Minde, alisema imefika wakati wa kila mtu kuacha ya ulimwengu na kutafuta suluhisho la kudumu kwa Mungu ili kuepuka matatizo yanayojitokeza kwenye jamii.

Alisema mwaka 2025 ni mwaka wa matumaini kwa kila mmoja atakayemtegemea Mungu na kufanya matendo yaliyomema kwa wenzake.

Askofu wa Jimbo Katoliki la Kahama mkoani Shinyanga, Mhashamu Christopher Ndizeye alisema baada ya kupata madaraka ya uongozi wa udiwani na ubunge wanarudi kanisani kuungama, hivyo mambo hayo wanatenda makusudi kwa uchu wa madaraka.

Alisema, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa baadhi ya maeneo ulighubikwa na vurugu zilizosababisha kuwapo kwa uvunjifu wa amani na baadhi ya wananchi walipoteza maisha na kuishauri serikali kutatua changamaoto zilizojitokeza kabla ya kuingia kwenye uchaguzi mkuu.

Askofu Msaidizi wa Jimbo Kuu Katoliki la Dodoma, Wilbroad Kibozi, aliwataka Watanzania kuweka mikakati ya kusaidia watu wasiojiweza, ili waweze kupiga hatua katika shughuli wanazofanya.

Alisema hayo wakati wa maadhimisho ya misa takatifu ya mkesha wa mwaka mpya iliofanyika katika Kanisa Kuu Katoliki la Paulo wa Msalaba Jimbo Kuu la Dodoma.

Askofu Mkuu wa Kanisa la Karmeli Assembleis of God Tanzania Dk. Evance Chande, alisema kwenye Uchaguzi Mkuu 2025, Watanzania wasikubali kuwachagua wagombea wanaojihusisha na vitendo vya kishirikina na watakao tumia rushwa kutaka kuingia madarakani.

Mchungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Ng'ambo ya Mto Pangani, Warehema Chamshana amesema mwaka huu ni wa Uchaguzi Mkuu, hivyo Watanzania waendelee kuomba kutokana na kwamba ni jambo kubwa kwa mustakabali wa maendeleo ya nchi.

Pia, aliwataka Watanzania kujitokeza kwa wingi kujiandikisha kwenye Daftari la Wapigakura ili kuweza kupata ridhaa ya kuwachagua viongozi ambao watawaongoza katika kipindi cha miaka mingine mitano.

Askofu wa Kanisa Katoliki Jimbo la Mbulu, Antony Lagwen, amewaonya viongozi wenye uchu wa madaraka na mali kuacha kwa kuwa ndicho chanzo cha kupotea kwa amani, huku akiwatwisha mzigo wasomi kutetea haki za watu.

Alisema mara nyingi amani inapokosekana binadamu wenye uchu wa madaraka na uchu wa mali ndiyo hutumia nafasi hiyo.

Pia, alitumia fursa hiyo kuwataka wasomi kusaidia watu kujua haki zao na kutetea haki za wananchi ili watu wazitambue.

***Imeandaliwa na Elizabeth Zaya (Dar), Mary Mosha (Moshi), Shabani Njia (Kahama), Renatha Msungu (Dodoma), Peter Mkwavila (Dodoma), Osca Asenga (Tanga), Jaliwason Jasson (Manyara). Marco Maduhu (Shinyanga), Rose Jacob na Vitus Audax (Mwanza)**

# Ulega ampa maua Samia ujenzi barabara

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan ameridhia kuanza kwa ujenzi wa barabara ya Mbagala hadi Kongowe itakayopunguza foleni upande wa Kusini mwa Dar es Salaam.

Barabara hiyo itafungua fursa za kiuchumi kwa mikoa ya Kusini na kuondoa kero ya muda mrefu katika eneo la Mbagala hadi Kongowe, ikiwa ni mpango wa kitaifa wa Rais Samia kuboresha miundombinu nchini.

Waziri wa Ujenzi, Abdallah Ulega, jana akitangaza kuanza kwa mchakato wa upanuzi foleni ukanda huo, katika viwanja vya Shule ya Msingi Mwandege, mkoani Pwani jana, alisema kipande cha barabara kitakachopanuliwa kwa muda mrefu kimekuwa kero kwa wananchi kwa kusababisha foleni za muda mrefu.

"Naomba kuwaambieni leo kwamba Rais amekubali ombi letu la kufanya upanuzi wa barabara hiyo na ameruhusu taratibu za zabuni kuanza. Sasa kero hii inakwenda kumalizika haraka na shughuli zenu za kiuchumi na kijamii sasa zitapata kasi mpya, alisema Ulega.

**"Naomba kuwaambieni leo kwamba Rais amekubali ombi letu la kufanya upanuzi wa barabara hiyo na ameruhusu taratibu za zabuni kuanza. Sasa kero hii inakwenda kumalizika haraka ...**

Alikuwa akizungumza katika Mkutano mkuu wa mwaka wa Jimbo la Mkuranga ambalo ni mbunge. Mkutano huo hufanyika mwishoni mwa mwaka kutokana na utaratibu ambao amejiwekea tangu awe mbunge.

Alipoteuliwa kuwa Waziri wa Ujenzi mwezi Desemba, mwaka jana, alisema ujenzi wa barabara hiyo kuanzia eneo la Kokoto - Mbagala Rangi Tatu kuelekea Kongowe ni sehemu ya ujenzi mkubwa wa barabara unaoendelea nchini kote chini ya utawala wa Rais Samia.

Alisema kwamba mafanikio katika ujenzi wa barabara, madaraja, miradi ya umeme na mambo mengine unatokana na mafanikio ya kiuchumi ambayo Tanzania imeyapata kwenye utawala wa Rais Samia.

"Waswahili wanasema usione vyaelea vimeundwa. Huwezi kujenga barabara namna hii, ukajenga Bwawa la Mwalimu Nyerere, ukajenga SGR bila kuwa na uchumi unaoruhusu hayo. Rais wetu ni wa kipekee na maono na miongozo yake ndiyo inafanya tutambe namna hii," alisema.

Aidha, mwenendo wa kiuchumi unaoendelea sasa, kuna uwezekano wa kero nyingi za barabara kupungua sana wakati wa utawala wa Rais Samia na kusema anatarajia atapata kura nyingi kutoka kwa Watanzania kwenye uchaguzi wa mwaka 2025 kwa sababu rekodi yake inajieleza.

Katika mkutano huo ambao mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, baadhi ya viongozi waliohudhuria walikuwa ni madiwani, wenyeviti wa mitaa na viongozi wengine wa chama na serikali katika Wilaya ya Mkuranga na Mkoa wa Pwani kwa ujumla.

Pamoja na mambo mengine, Ulega alieleza mafanikio makubwa ambayo yamepatikana katika wilaya hiyo ikiwamo ongezeko la shule za msingi, vituo vya afya na kuimarika kwa huduma za kijamii.

Mbele ya wananchi wa Mkuranga, Ulega alitangaza pia kuanza kwa ujenzi wa jengo la ghorofa litakalotumika kufundisha wanafunzi katika Shule ya Msingi Mwandege.

Alisema hatua hiyo imezingatia ukweli kwamba eneo la Mwandege lina idadi kubwa ya watu na kwa ukubwa wa eneo iliko sasa, namna pekee ya kukabiliana na ongezeko la wanafunzi ni kujenga shule za ghorofa zitakazotumia eneo dogo kusomesha wanafunzi wengi zaidi.



Taka zikiwa zimerundikwa mbele ya maduka mjini Mugumu Serengeti mkoani Mara jana kutokana na kilichoelezwa kuwa mzabuni kugoma kuzoa kwa madai ya kutolipwa fedha zake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Kenya, Tanzania wafunga mwaka kwa ujirani mwema

**Na Ambrose Wantaigwa,** TARIME

MBUNGE wa Jimbo la Kurya Magharibi nchini Kenya, Mathias Rhobi, amesema amani na usalama katika nchi ya Tanzania ni mfano wa kuigwa katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Aliambatana na viongozi wenzake kuhudhuria hafla ya kufunga mwaka ya ujirani mwema iliyoandaliwa na wazee na viongozi kutoka pande zote (Kenya na Tanzania), mjini Tarime.

"Ninashukuru wenzangu kutoka Tanzania kuendelea kuimarisha amani na usalama katika nchi yao hatua ambayo inasababisha nchi zote jirani kuwa salama na kuzuia uhalifu katika maeneo ya mipakani," alisema.

Alisema Tanzania imeweza kubadilisha uongozi awamu sita kwa njia za amani kupitia uchaguzi unaofanyika bila vurugu na uharibifu wa mali.

Viongozi hao walijadiliana kuhusu namna ya kuepuka migawanyiko ya kikanda na vurugu wakati wa uchaguzi na mbinu za kuzuia uhalifu wa mipakani.

Mkuu wa Wilaya ya Tarime, Edward Gowele, alisisitiza umuhimu wa wanasiasa kushirikiana kuimarisha usalama kwa kuwa ndio msingi wa kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo ya wananchi.

"Wanasiasa wa pande zote wanapaswa kutumia nafasi zao kuhubiri amani na utengamano kwa kuwa ndio msingi wa kuwezesha serikali yoyote kutekeleza miradi na kuboresha maisha ya watu wake," alisema.

Mbunge wa Viti Maalum kutoka Mkoa wa Mara, Esther Matiko (CHADEMA), alisema mikakati ya kuimarisha ulinzi na usalama katika eneo hilo halina itikadi ya vyama na kuwataka wananchi kuepuka migawanyiko kutokana na itikadi zao.

# Kapufi: Viongozi wenye kampuni ujenzi wasiombe zabuni za miradi

**Mussa Mwangoka**, KATAVI

MBUNGE wa Mpanda Mjini, Sebastian Kapufi amewashauri viongozi wa kisiasa wakiwamo wabunge, wenyeviti wa halmashauri na madiwani wenye kampuni za ujenzi kutokuwa sehemu ya waombaji wa zabuni za miradi ya maendeleo ya halmashauri husika.

Amesema wakishiriki watakuwa wanaathiri utekelezaji wa miradi hiyo na thamani ya fedha iliyotolewa inashindwa kuonekana katika miradi husika inapokamilika.

Alitoa ushauri huo juzi alipokuwa katika ziara ya kikazi iliyolenga kukagua miradi ya maendeleo iliyofanyika katika kata zote za Jimbo la Mpanda mjini, mkoani Katavi.

Kapufi alisema wananchi wanatamani kuona kuna uwiano sawa wa fedha zilizotolewa na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri hiyo ambayo serikali imepeleka zaidi ya Shilingi bilioni sita katika msimu wa fedha wa mwaka 2024/25.

"Mathalani imetolewa Sh. milioni 600 kwenye ujenzi wa mradi wa shule ya sekondari ni vyema hata mwananchi wa kawaida akaona thamani ya mradi huo ikifanana na fedha zilizotumika sio kuwapo na ujanja ujanja ambao unafanya miradi mingi kutekelezwa chini ya kiwango," alisema.

Kadhalika, viongozi hawapaswi kuwa sehemu ya washiriki katika shughuli hizo, kwa kuwa kufanya hivyo kutafanya washindwe kutimiza wajibu wao wa kusimamia utekelezaji wa miradi hiyo.

Kauli ya Kapufi inakuja wakati baadhi ya viongozi wa kisiasa ni miongoni mwa wamiliki wa kampuni za ujenzi na wamekuwa wakitajwa kushinda zabuni za utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo, ambayo mingine ikilalamikiwa kutekelezwa chini ya kiwango.

Awali, Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa ya Mpanda, Leonard Kilamhama, alisema serikali imetoa Sh. bilioni 4.7 kwa ajili ya ujenzi wa shule mbili za Shanwe na ya kanda itakayochukua wanafunzi kutoka mikoa ya Katavi, Kigoma na Tabora.

Kilahama alisema kukamilika kwa ujenzi wa shule hizo kutasaidia kupunguza tatizo la wanafunzi kukosa nafasi za masomo wanapofaulu mitihani yao ya mwisho ya kumaliza elimu ya msingi.

# Kicheko petroli, dizeli ikishuka bei

**Na Mwandishi Wetu**

BEI ya mafuta ya petroli na dizeli ya rejareja kwa Januari 2025 imeendelea kushuka nchini, ikilinganishwa na Desemba mwaka jana, huku sababu kubwa ikitajwa ni kupungua kwa viwango vya kubadilishia fedha za kigeni.

Taarifa iliyotolewa jana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) kupitia Mkurugenzi Mkuu wake, Dk. James Mwainyekule, ilisema kuwa bei za mafuta kuanzia jana kwa yanayochukuliwa Bandari ya Dar es Salaam, petroli imeshuka kutoka Sh. 2,898 iliyokuwa ikiuzwa Desemba kwa lita moja hadi Sh. 2,793 itakayouzwa kipindi cha Januari.

Taarifa hiyo ilisema kuwa petroli inayochukuliwa katika Bandari ya Tanga, lita moja imeshuka kutoka Sh. 2,905 iliyokuwa ikiuzwa Desemba hadi Sh. 2,800 kwa lita itakayouzwa Januari na kwa Bandari ya Mtwara pia imeshuka kutoka Sh. 2,908 ya Desemba hadi Sh. 2,866.

Bei ya dizeli, taarifa ya EWURA ilisema kuwa bidhaa hiyo inayopokewa Bandari ya Dar es Salaam imeshuka kutoka Sh. 2,779 ya Desemba hadi Sh. 2,644.

Dizeli inayopokewa katika Bandari ya Tanga imeshuka kutoka Sh 2.792 ya Desemba hadi Sh. 2,656 na Bandari ya Mtwara imeshuka kutoka Sh. 2,851 iliyokuwa ikiuzwa Desemba hadi Sh. 2,716, Januari kwa lita.

"Gharama za mafuta (FOB) na gharama za uagizaji (Premiums) zinalipiwa kwa kutumia fedha za kigeni ikiwamo Dola ya Marekani. Kwa bei za Januari 2025, wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni umepungua kwa asilimia 11.27," ilisema taarifa hiyo.

Aidha, taarifa hiyo ilitaja sababu nyingine kuwa ni bei za uagizaji wa mafuta hayo kusababisha kupungua bei.

"Gharama za uagizaji mafuta zimeongezeka kwa wastani wa asilimia 5.45 kwa petroli, asilimia 13.01 kwa dizeli na wastani wa asilimia 8.82 kwa mafuta ya taa katika Bandari ya Dar es Salaam; zimepungua kwa asilimia 6.67 kwa petroli na asilimia 6.67 katika Bandari ya Tanga; na zimepungua kwa wastani wa asilimia 4.61 kwa mafuta ya petroli na asilimia 10.33 kwa mafuta ya dizeli katika Bandari ya Mtwara."

# TRA yavuka lengo yakusanya Tril. 3.5/-

**Na Restuta James**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imevuka lengo la makusanyo ya kodi kwa asilimia 103.52 mwezi uliopita, kwa kukusanya Sh. trilioni 3.587, huku ikiweka maazimio nane ya kuongeza ufanisi wa utendaji wake kwa mwaka 2025.

Aidha, sekta za madini, benki, uzalishaji viwandani na biashara, ndizo zilizowezesha makusanyo hayo.

Akizungumza na waandishi wa habari Dar es Salaam jana, Kamishna Mkuu wa TRA, Yusuf Mwenda, alisema makusanyo hayo yameiwezesha mamlaka hiyo kukusanya Sh. trilioni 16.528 sawa na asilimia 104.7, katika kipindi cha nusu mwaka wa fedha 2024/2025 cha Julai hadi Desemba 2024.

Alisema makusanyo hayo ni kiwango cha juu kuwahi kufikiwa na TRA, ikilinganishwa na nusu ya mwaka wa fedha 2023/2024, mamlaka hiyo ilikusanya Sh. trilioni 13.9.

"Makusanyo haya ni sawa na ongezeko la asilimia 78.78 toka Sh. trilioni 9.242 zilizokusanywa katika kipindi kama hichi mwaka wa fedha 2020/2021 kabla ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan," alisema Mwenda.

Kamishna Mwenda alisema kwa Desemba TRA imevunja rekodi kwa kuongeza ukuaji wa mapato kwa asilimia 17.59 kutoka makusanyo ya Sh. trilioni 3.050 Desemba 2023 hadi Sh. trilioni 3.587 mwaka jana. Alisema kwa robo ya pili ya mwaka jana (Oktoba hadi Desemba), TRA ilikusanya Sh. trilioni 8.741 sawa na asilimia 104.63, ikiwa ni ukuaji wa asilimia 19.05 ikilinganishwa na Sh. trilioni 7.342, zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2023.

Pamoja na mambo mengine, TRA imefuatilia kwa ukaribu hali ya ufanyaji wa biashara nchini, kwa kusimamia uzalishaji viwandani pamoja na kuhimiza matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD).

Kuhusu sekta zilizoibeba TRA, Kamishna wa Walipakodi wakubwa, Michael Muhoja, alisema ni ya fedha ikiongozwa na benki, madini, uzalishaji viwandani na biashara.

Katika makusanyo ya Sh. trilioni 3.587 ya Desemba 2024, Sh. trilioni 1.660 zimelipwa na benki, wakati biashara na tozo za forodha zikichangia Sh. trilioni 1.100 na kiasi kilichobaki kikilipwa na madini pamoja na uzalishaji viwandani.

Alisema ili kuongeza makusanyo, TRA inaweka mkakati wa kuongeza idadi ya walipakodi wakiwamo wadogo, wa kati na wakubwa.

Akizungumzia mfumo wa IDRAS, Kamishna wa Kodi za Ndani, Alfred Mregi, alisema wameongeza sehemu ya kutunza kumbukumbu ya bidhaa zinazozalishwa nchini, ili kurahisha ukadiriaji wa kodi kwa viwanda vya ndani.

Lengo ni kupunguza malalamiko ya wafanyabiashara kubambikiwa kodi, kwa kuwa taarifa zinazoingizwa kwenye mfumo ndizo zitakazowezesha ukadiriaji wa kodi.

Akizungumzia mfumo wa TANCIS, Kamishna wa Forodha, Juma Hassan Bakari, alisema umeboreshwa na kuongeza taasisi nyingi zaidi ukiwamo Wakala wa Barabara (TANROAD), viwanja vya ndege na ofisi za mipaka ya nchi, ili kuwarahisishia wafanyabiashara huduma.

Kuhusu maazimio nane, Kamishna Mwenda alisema mamlaka hiyo inalenga kukusanya Sh. trilioni 30.04 katika mwaka huu wa fedha 2024/2025; na kwamba wanakuhamasisha ulipaji wa kodi wa hiari, kuanza kutumia mifumo iliyoboreshwa, kuimarisha uhusiano wake na walipakodi na matumizi ya EFD.

Mengine ni kuweka mazingira sawa ya biashara kwa kuweka mifumo ya haki na sawa ya utozaji wa kodi, kushirikiana na timu iliyoindwa na Rais Samia ya kufanya mapitio ya kodi, kuimarisha huduma kwa walipakodi na vitengo vya ukaguzi na uchunguzi wa kodi ili kuzuia ukwepaji wa kodi.

***Kwa maoni: +255 677 020 701 Email: customerrelations@guardian.co.tz***




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaokopa taasisi zisizo rasmi zingatieni ushauri wa BoT

**KUMEKUWA** na vilio na malalamiko huku baadhi ya watu kufikia hatua ya kupoteza maisha kutokana na kujiingiza kwenye mikopo ambayo inatolewa na taasisi zisizo rasmi.

Baadhi ya wananchi huingia kwenye mikopo hiyo kwa kushawishiwa na taasisi hizo kwa maneno matamu ili kuvutia wateja kukopa huku lengo lao likiwa kuwakamua wakopaji hao.

Kuna wanaoingia kwenye mikopo hiyo kwa kutafuta njia rahisi ya kupata fedha kwa haraka badala ya kufuata njia sahihi zinazotolewa na benki zinazotambulika.

Matokeo yake ni wakopaji hao kudhalilishwa kwa kunyang'anywa samani zao na wengine nyumba zao kupigwa mnada na baadhi kutokana na udhalilishaji huo hupata msongo wa mawazo na kujitoa uhai.

Kinamama ni waathirika wakubwa wa mikopo hiyo kutokana na shughuli zao za ujasiriamali wakitaka kuongeza mitaji kwa kujaribu kukopa, lakini huishia kufilisiwa mali zao.

Viongozi mbalimbali wa kisiasa kila mara wanatoa tahadhari wananchi kujiepusha na mikopo hiyo ambayo kwa jina maarufu hujulikana kama 'mikopo umiza', lakini kama wahenga wanavyosema sikio la kufa halisikii dawa.

Ili kuwaepusha wananchi na kadhia hiyo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imepiga marufuku taasisi zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo bila kuwa na leseni inayotambulika kisheria.

BoT imetoa marufuku hiyo baada ya kubainika uwapo wa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma ya kifedha hususani ya mikopo bila ya kutambulika kisheria kuendelea kutoa huduma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, huduma hizo za kifedha zinatakiwa zitolewe na taasisi ambazo tayari zimepewa leseni ya kufanya kazi hiyo.

Kwa mujibu Tutuba, Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, ni kosa kwa taasisi, kampuni na watu binafsi kujihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila kuwa na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 16(2)(a) cha sheria hiyo kimeainisha adhabu inayopaswa kutolewa kwa kuendesha biashara ya kukopesha bila kuwa na leseni ikiwa ni pamoja na kutozwa faini isiyopungua Sh.milioni 20 au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja.

"Hivyo basi, Benki Kuu inapenda kuusisitiza umma kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambaye hana leseni."


"Endapo taasisi au mtu binafsi anataka kufanya biashara ya ukopeshaji, anatakiwa kufuata taratibu husika za kuomba leseni kutoka BoT ili apewe kwa mujibu wa sheria. Ni muhimu mtu anapotaka kukopa, atumie taasisi zenye leseni ya BoT ili kuhakikisha kuwa huduma anayopata ni salama na inayozingatia sheria za nchi."

Benki hiyo pia imeshangazwa na uwapo wa taarifa katika mitandao ya kijamii zinazohusisha alama za wanyama kama vile kobe na nyoka katika utoaji wa mikopo na kwamba jambo hilo ni kinyume cha sheria na maadili ya utoaji huduma za kifedha.

"Wananchi wanashauriwa kupuuza taarifa hizo na kutokujihusisha nazo kwa kuwa hazijapewa leseni hapa nchini."

Wananchi kama wanataka huduma hiyo ya kifedha, wameshauriwa watumie taasisi zenye leseni za kukopesha zilizoidhinishwa na BoT pamoja na zenye leseni za mikopo ya kidijitali ambazo zipo kwenye tovuti ya benki hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Muungwana Lazima Nilonge



Na Mwandishi Wetu

# Mwaka 2025 ukuweke mama mbali na kashfa uvutaji bangi

**MWAKA** uliopita ulibainika kuwa na ongezeko kubwa la wanawake wanaovuta bangi, ikidaiwa lengo lao ni kuwapunguzia msongo wa mawazo.

Mbali na lengo hilo, wengine walijihusisha na uvutaji bangi, kutokana na migogoro ya kimapenzi, pia kutumia kilevi hicho kama starehe, pasipo kujali madhara yake kiafya.

Kamishna Jenerali Aretas Lyimo, akiwasilisha taarifa ya operesheni ya kusaka dawa za kulevya iliyofanyika nchi nzima kati ya Oktoba na Novemba mwaka jana.

Anataja bangi aina ya 'skanka' inayosemekana kuwa na kiwango kikubwa cha sumu kali, lakini wanawake ndio wanaitumia bila ya hofu.

Nimegusia kidogo hali ilivyokuwa mwaka jana, ili kuwakumbusha wanawake kuwa tunapoanza mwaka mpya wa 2025, tutambue madhara ya kilevi hicho na umuhimu wa kuachana nacho.

Tuingie mwaka mpya na mambo mapya hasa kwa kuanza maisha mengine yasiyogusa bangi ili kulinda afya, kwani wataalamu wa afya wanasema uvutaji huo, husababisha madhara makubwa katika mapafu ya mvutaji.

Vilevile kuna kero ya kama kukohoa na koo kuwasha na kwamba, uvutaji huo wa bangi unamweka mvutaji katika hatari mara tano zaidi ya kupata saratani ukilinganisha na mvutaji sigara.

Pia, kuna haja ya kusonga mbali zaidi kuwa, licha tu ya matatizo ya ubongo yanayoathiri afya ya akili kwa mvutaji, bado inaangukia kundi kwamba, ni ugonjwa mbaya unaowapata wavutaji bangi.

Kwa kifupi, anayevuta bangi huwa na uwezo mdogo wa kumbukumbu. Uvutaji wa hizo dawa za kulevya, humwondolea mtu uwezo wa asili wa kufanya maamuzi sahihi, akilinganishwa na mtu asiyejihusisha na matumizi ya bangi.

> **Tuingie mwaka mpya na mambo mapya hasa kwa kuanza maisha mengine yasiyogusa bangi ili kulinda afya, kwani wataalamu wa afya wanasema uvutaji huo, husababisha madhara makubwa katika mapafu ya mvutaji.**

Hivyo, ili kuondokana na madhara hayo, ni vyema kutojihusisha na uvutaji wa dawa hizo zenye madhara makubwa kiafya.

'Ukiwa bado ni mbichi' tukitumia lugha ya mtaani, ni kwamba mwaka 2025 uwe ni watu kuwa huru, kutoka katika kifungo cha matumizi ya bangi. Ni kwamba, mtumiaji anapovuta msokoto huo, anaanza kufanya kazi baada ya dakika chache na yeye huanza kuhisi mapigo ya moyo yakienda mbio.

Kwa kuwa mvutaji, pia huanza kubadilika na kuona vitu visivyo katika uhalisia kutokana na maruweruwe: Matokeo ya muda mfupi baada ya kuvuta moshi, basi wale wote wanaojihusisha na wengine wanaotamani, ni vyema wakaacha.

Wanaitumia dawa hizo za kulevya kama njia ya kuondoa msongo wa mawazo, wakumbuke kuwa wanahatarisha afya zao.

Kwanini tuendekeze mabaya haya, dhidi ya tija zetu kiafya? Kwa watu wenye msongo wa mawazo au migogoro ya kimapenzi, jambo jema kwao ni kuwaona washauri nasaha au wataalamu wa saikolojia.

Hatua hiyo ije na mapya yake, iwe ya kuweka sawa kwa ajili ya kulinda afya zao badala ya kuziangamiza kama njia ya kupata unafuu katika migogoro.

Ninaamini kwamba anaweza kuwaweka sawa watu wenye matatizo hayo, sio kutegemea dawa za kulevya, ambazo kimsingi ni hatari kwa watumiaji na pia zinaweza kuwaweka matatani pale wanapobainika kujihusisha.

Vilevile, wanaotumia bangi kama starehe, ni vyema nao wakatumia vitu ambavyo havina madhara kiafya, kwa sababu kuvuta dawa hizo sio starehe bali ni kujiangamiza bila kujua.

HABARI KITAIFA

# Wakulima wa korosho wavuna bil.360/-

**Na Hamisi Nasri,** MTWARA

MKUU wa Wilaya ya Mtwara, Abdallah Mwaipaya amehitimisha minada 12 ya korosho ya Chama Kikuu cha Ushirika Masasi, Mtwara na Nanyumbu (MAMCU), huku tani 116,824 za korosho ghafi zikiuzwa na kuwaingizia wakulima zaidi ya Sh. bilioni 360.

Akizungumza wakati wa mnada huo, Mwaipaya alisema fedha za korosho walizopata wakulima katika msimu wa mwaka 2024/2025 ni nyingi na kuwataka wazitumie kufanya mambo ya maendeleo.

Mwaipaya alisema moja ya mambo ya msingi ambayo wakulima wanapaswa kuyazingatia katika matumizi ya fedha hizo ni pamoja na kuwasomesha watoto wao.

Alisema shule zitafunguliwa hivi karibuni, wakulima wanapaswa kuanza kufanya maandalizi ya mahitaji ya watoto kwa kutumia fedha hizo.

"Zaidi ya tani 116,825 za korosho za MAMCU zimeuzwa katika minada 12 na wakulima wamepata mabilioni ya fedha nawaomba zitumieni katika mambo ya kimaendeleo," alisema.

Meneja Mkuu wa MAMCU, Biadia Matipa, alisema mnada huo ndio wa mwisho kufanyika katika msimu huu wa korosho mwaka 2024/2025.

Alisema wakulima wameingiza zaidi ya Sh. bilioni 360 kati ya minada 11 ambayo tayari wamelipwa.

Matipa alisema kumalizika kwa minada ya korosho msimu huu MAMCU kinaingia katika maandalizi ya misimu ijayo ya mbaazi, choroko, ufuta na korosho na bei pia zitakuwa nzuri katika msimu ujayo.

"Leo ndio tunafunga minada ya korosho, huu ndiyo mnada wa mwisho kwa MAMCU msimu huu ambapo hadi sasa tumeuza zaidi ya tani, 116,825 ndani ya msimu huu ni mafanikio makubwa sana ukilinganisha misimu ya nyuma ambapo mauzo yalikuwa ni chini ya hapo."

Mmoja wa wakulima wa korosho kutoka Mtwara-Mikindani, Musa Rashidi, alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Abdallah Mwaipaya kwa ushauri alioutoa wa matumizi sahihi ya fedha walizopata za mauzo ya korosho.



Mkuu wa Wilaya ya Mtwara, Abdallah Mwaipaya (kushoto), akiangalia karatasi ambayo inamwenendo wa mauzo ya minada ya zao la korosho kwa chama kikuu cha ushirika wa wakulima Mtwara, Masasi na Nanyumbu (MAMCU) wakati wa kuhitimisha mnada wa mwisho wa chama hicho, Mikindani, Mtwara jana. Kulia ni Meneja Mkuu wa MAMCU, Biadia Matipa. **PICHA: HAMISI NASRI**

# BoT yapiga marufuku mikopo 'kausha damu'

**Na Elizabeth Zaya**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT) imepiga marufuku taasisi zinazojishughulisha na utoaji wa mikopo bila kuwa na leseni inayotambulika kisheria.

Taarifa hiyo imetolewa baada ya kubainika uwapo wa baadhi ya taasisi zinazotoa huduma ya kifedha husussani ya mikopo bila ya kutambulika kisheria kuendelea kutoa huduma hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi na Gavana wa BoT, Emmanuel Tutuba, huduma hizo za kifedha zinatakiwa zitolewe na taasisi ambazo tayari zimepewa leseni ya kufanya kazi hiyo.

Kwa mujibu Tutuba, Kifungu cha 16(1) cha Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya Mwaka 2018, ni kosa kwa taasisi, kampuni na watu binafsi kujihusisha na biashara ya kutoa mikopo bila kuwa na leseni kutoka Benki Kuu ya Tanzania.

Aidha, Kifungu cha 16(2)(a) cha sheria hiyo kimeainisha adhabu inayopaswa kutolewa kwa kuendesha biashara ya kukopesha bila kuwa na leseni ikiwa ni pamoja na kutozwa faini isiyopungua Sh.milioni 20 au kifungo cha muda usiopungua miaka miwili au vyote kwa pamoja.

"Hivyo basi, Benki Kuu inapenda kuusisitiza umma kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambaye hana leseni," alisema Tutuba kupitia taarifa yake kwa umma.

> **"Hivyo basi, Benki Kuu inapenda kuusisitiza umma kuepuka kukopa au kufanya biashara na taasisi, kampuni au mtu binafsi ambaye hana leseni," alisema Tutuba kupitia taarifa yake kwa umma.**

"Endapo taasisi au mtu binafsi anataka kufanya biashara ya ukopeshaji, anatakiwa kufuata taratibu husika za kuomba leseni kutoka BoT ili apewe kwa mujibu wa sheria. Ni muhimu mtu anapotaka kukopa, atumie taasisi zenye leseni ya BoT ili kuhakikisha kuwa huduma anayopata ni salama na inayozingatia sheria za nchi."

Kadhalika, alishangazwa na uwapo wa taarifa katika mitandao ya kijamii zinazohusisha alama za wanyama kama vile kobe na nyoka katika utoaji wa mikopo na kwamba jambo hilo ni kinyume cha sheria na maadili ya utoaji huduma za kifedha.

"Hivyo, wananchi wanashauriwa kupuuza taarifa hizo na kutokujihusisha nazo kwa kuwa hazijapewa leseni hapa nchini."

Aliwataka wananchi kama wanataka huduma hiyo ya kifedha, watumie taasisi zenye leseni za kukopesha zilizoidhinishwa na BoT pamoja na zenye leseni za mikopo ya kidijitali ambazo zipo kwenye tovuti ya benki hiyo.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Samia afurahia Mwaka Mpya na wazee

**Na Steven William,**
MUHEZA

RAIS Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa zawadi ya chakula cha Sikukuu ya Mwaka Mpya katika kituo cha wazee cha Misufini, wilayani Muheza.

Akikabidhi zawadi hizo juzi kwa niaba ya Rais, Katibu Tawala Wilaya ya Muheza, Mohamed Mfaki, alisema zawadi hizo zimelenga kusherehekea sikukuu ya Mwaka Mpya.

Zawadi hizo ni mchele, kuku, sabuni, maji, soda, juisi, mafuta ya kupikia na viungo vya mboga.

Alisema wakati huu ambao wananchi wengi wapo katika maandalizi mbalimbali kwa ajili ya kusherehekea mwaka mpya, Rais ameona ipo haja ya kuwakumbuka wazee waweze kufurahia siku hiyo.

Alisema serikali inalengo kubwa la hudumia wazee vyakula, malazi na matibabu.

Alisema ndio maana Rais amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya kila sikukuu wazee wapatiwe chakula na pia wajiorodheshe kwa ajili ya kupatiwa mkopo fedha kuendelea miradi yao.

Kadhalika, serikali itawaboreshea kituo hicho cha Misufini ikiwamo kujengewa nyumba ili walale pazuri.

Aliwaagiza wazee wasipange foleni wanapokwenda kupata matibabu na huduma iwe bure za afya kwa kuwa walishatumikia taifa.

Mzee anaelelewa katika kituo hicho, Joseph Misigalo, amemshukuru Rais Samia, viongozi wa wilaya na mkoa kwa zawadi hizo na kumwombea kwa Mungu aendelee kumlinda na kumwongoza katika uongozi wake.

"Tupelekee salamu zetu sisi wazee tunamwombea kwa Mungu katika vipindi vya utawala wake akulinde ili uweze kuendelea kutufanyia yaliyo mazuri zaidi," alisema Misigalo.

Aliomba huduma kwa wazee ziboreshwe kila hospitali wanazokwenda kutokana na nyingine kukataliwa kupewa matibabu.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Fani Mussa, alisema wazee 13,829 wilayani Muheza wametambuliwa na kupatiwa vitambulisho vya msamaha wa matibabu.

Alisema kuwa hadi kufikia Novemba 2024 jumla ya wazee 13,829 wilayani humo wametambuliwa na kupatiwa vitambulisho vya msamaha wa matibabu.

Alisema kati ya wazee hao wanaume 7,160 na wanawake ni 6,667 lengo ni kuhakikisha wazee wanapata huduma kwa wakati.

Alisema kuwa kuhakikisha wazee wanapatiwa matibabu kwa wakati wamepewa kipaumbele cha kwanza katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa kufuata utaratibu wa Mpishe Mzee Apate Huduma Kwanza.

Fani alisema kuwa wazee hao wamekuwa wakipata huduma mbalimbali ikiwamo kupima Afya zao mara moja kila mwezi.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Issa Msumari, alisema kuwa wazee wanamshukuru Mungu kwa kufikia mwaka 2025 na wanatakiwa kuendelea kumuomba Mungu.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mfawidhi Kituo cha Misufini, Mwamvita Kilima, alisema kambi hiyo inawahudumia wazee 17 na wanawake wanne na wanaume 13.

Alisema kuwa kituo kimepata mafanikio kujenga bweni, kukarabati barabara kuna umeme na maji, kupima macho wazee, sukari na wamepatiwa bima ya afya pamoja na chakula.

Hata hivyo, waliomba kujengewa jiko, bwalo, ofisi na nyumba ya mtumishi na kupatiwa gari kwa wazee wenye ulemavu.



Madereva wa bajaji wakiwa kwenye foleni ya kujaza gesi kwa saa zaidi ya saba wakisubiri kupata huduma hiyo katika kituo cha Tabata jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Jamii yaombwa kuwakumbuka watoto wenye mahitaji

**Na Grace Mwakalinga**

ZAIDI ya watoto 30 waliofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia wanalelewa katika vituo vya watoto yatima vilivyopo Manispaa ya Kigamboni, jijini Dar es Salaam.

Watoto hao, ambao wamepitia mateso ya kubakwa na kupigwa na wazazi au walezi wao, sasa wanapatiwa huduma na wasamaria wema kupitia uongozi wa Serikali za Mitaa na Ustawi wa Jamii.

Kikundi cha Wajomba Family cha Kigamboni, kimechanga fedha ili kununua mahitaji muhimu kwa watoto hao ili kusherehekea sikukuu ya kuvuka mwaka.

Mwenyekiti wa Kikundi cha Wajomba Family, Salum Ally Ramadhan, jana alisema kuwa wameamua kusaidia watoto yatima kutokana na mazingira magumu wanayoishi.

"Kila mwaka tunachangishana fedha na kutoa misaada ya vyakula, nguo, mafuta ya kupikia, maji ya kunywa, na mahitaji mengine muhimu. Kigamboni kuna vituo 10 vya watoto yatima na tunapanga kuvifikia vyote na kuhakikisha wanapata huduma zinazohitajika," alisema Ramadhan.

Katika kufunga mwaka 2024 na kuukaribisha mwaka 2025, kikundi cha Wajomba Family kimetoa misaada kwa vituo sita vya watoto yatima.

Alisema msaada huo unajumuisha chakula, mafuta ya kupaka, ya kula, maji ya kunywa na nguo ili watoto hao waweza kusherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya kwa furaha, kama watoto wengine.

Katika kusherehekea Mwaka Mpya, Ramadhan, amewaomba wazazi na walezi kuacha migogoro isiyokuwa na msingi ndani ya ndoa, ambayo alisema ni chanzo cha kusababisha ukatili wa kijinsia kwa watoto na kuishia kulelewa katika vituo.

Alisema, ili kudhibiti hali hiyo ni muhimu serikali isimamie Sheria ya Ndoa ya mwaka 2019 na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 kwa kuhakikisha haki za watoto zinaheshimiwa.

Mlezi wa Kituo cha Hisani Orphanage Centre kilichopo Kibada, wilayani Kigamboni, Moza Omary, alisema kituo hicho kinahudumia watoto 84, kati yao wasichana 52 na wavulana 32.

Alisema watoto hao ni waliokumbwa na vitendo vya ukatili wa kijinsia, waliotoka katika familia maskini na wengine ambao wamefiwa na wazazi wao.

Msimamizi wa Kituo cha Yerusalem, Elizabeth Moses, ameeleza kuwa wanahudumia watoto 32, wakiwamo wale waliotoka katika mazingira hatarishi na wale walioathirika na ukatili wa kijinsia.

Mlezi wa Kituo cha Amani, Sauda Hashim Juma, aliongeza kuwa wanahudumia watoto 56, kati yao wasichana 30 na wavulana 26, ambao pia ni yatima na waliokumbwa na mateso.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Maweni, Kata ya Mawenzi, Said Mzuwanda, aliomba wadau wengine kuiga mfano wa kikundi hicho kusaidia watoto wenye mahitaji maalum.

Alihimiza msaada wa aina hiyo ni sadaka inayompendeza Mungu na inatoa baraka kutoka kwa watoto hao, ambao wangeweza kuwa na familia bora, lakini mazingira yamewafanya wapigane na changamoto kubwa za maisha.

Alisema, wataendelea kuunga mkono juhudi za kikundi kwa kutembelea vituo vya watoto yatima mara kwa mara.

Shekhe Musa Omary, aliomba Wajomba Family kuwasaidia watoto hao kwa chakula na mavazi hasa wakati wa mwezi mtukufu wa Ramadhan, kipindi ambacho mahitaji ya misaada huwa ni makubwa zaidi.

# Hospitali Benjamin Mkapa kupandikiza figo kwa roboti

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

HOSPITALI ya Rufani Kanda ya Benjamin Mkapa (BMH), inatarajia kuongeza kasi ya upandikizaji figo kwa kutumia njia ya kisasa ya roboti ili kurahisisha matibabu kwa wagonjwa wa ndani na nje ya nchi.

Mkurugenzi Mtendaji wa BMH, Profesa Abel Makubi, alitangaza mpango huo kuwa ni moja ya mkakati wa hospitali hiyo kuboresha huduma za matibabu ya ugonjwa huo kwa mwaka huu.

Dk. Makubi alisema mwelekeo wa hospitali hiyo kwa mwaka huu ni kuongeza kasi ya utoaji huduma hizo kwa kutumia teknolojia za kisasa zaidi za upasuaji, uvunaji figo wa matundu madogo badala ya sehemu kubwa ya mwili.

Aidha, upasuaji wa kutumia roboti unarahisisha kazi kwa wataalamu wa kitengo cha wagonjwa wa figo ambao wanahitaji kufanyiwa upasuaji kutibu maradhi hayo.

"BMH imejipanga kufanya mambo makubwa kwenye sekta ya afya nchini na duniani hususani upandikizaji figo kwa wagonjwa wenye tatizo hilo kwa kutumia teknolojia ya kisasa," alisisitiza Profesa Makubi.

Alisema wanatarajia kufanya upanuzi kituo cha matibabu ya figo kiwe cha umahiri cha upandikizaji figo nchini na Afrika Mashariki na Kati kwa ufadhili wa Serikali ya Japan kwa kwa gharama ya takribani Sh. bilioni 33 kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

"Katika kituo hicho tutabobea zaidi katika utumiaji roboti kufanya upasuaji (Robotic Surgeries)," alisema.

Hospitali hiyo tangu ianze utoaji huduma za matibabu ya figo imepata mafanikio makubwa kutokana na wagonjwa wengi kupata matibabu, kuruhusiwa kurudi nyumbani na kuendelea na siku zao za kila siku za kujiingizia kipato.

Tangu kuanzishwa kwa huduma hiyo kwa mwaka jana, hospitali hiyo imepandikiza wagonjwa 14 figo na kuruhusiwa kutokana na afya zao kuendelea vizuri.

Miaka sita iliyopita, hospitali hiyo ilikuwa kituo cha pili nchini kuanza kutoa huduma hiyo.

Gharama za matibabu, serikali inatumia wastani wa Sh. milioni 34 kumtibu mgonjwa wa figo nchini badala ya Sh. milioni 64 nje ya nchi.

*Kwa maoni: +255 677 020 701*
*Email: customerrelations@guardian.co.tz*



# RC awaweka njia panda MADED, MADC K'njaro

**Na Mary Mosha,** SIHA

UJENZI wa vyumba vya madarasa kwa wakurugenzi wa halmashauri saba za Mkoa wa Kilimanjaro huenda ukageuka 'mwiba' kwao na kuwajibishwa iwapo watashindwa kukamilisha katika tarehe iliyopangwa.

Ni baada ya Mkuu wa Mkoa huo, Nurdin Babu kuweka mkazo kuwa anataka kuona ujenzi, ukarabati wa madarasa na mabweni katika shule zote unakamilika kabla ya Januari 11, mwaka huu kuruhusu wanafunzi kuingia darasani.

Taarifa ya Babu baada ya kukagua miradi hiyo katika shule sita zilizoko Wilaya ya Siha, Hai na Moshi, inaeleza hatamvumilia mkurugenzi wa halmashauri wala mkuu wa wilaya, atakayetoa sababu za kushindwa kutimiza agizo lake kwa tarehe iliyopangwa.

"Hakuna excuse (samahani), kwa kuwa tayari serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo hayo. Nataka yakamilike na viti na meza ziwekwe. Kilimanjaro hakutakuwa na mwanafunzi atakaye kaa chini," alisema huku akisisitiza kuwa: "Wakuu wa wilaya, watoto wote wanaopaswa kwenda shule waripoti shuleni, labda huyo mtoto awe amefariki dunia. Ila mambo ya mimba, sijui kutoroshwa, kukataa shule, sitaki kusikia, nitakuwa mkali sana juu ya hili." Alisema shule hizo zinapaswa kufungulia Januari 13, mwaka huu, na wanafunzi wote watapaswa kuingia darasani na kuendelea na masomo bila kisingizio chochote.

> **"Hakuna excuse (samahani), kwa kuwa tayari serikali imetoa fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa majengo hayo. Nataka yakamilike na viti na meza ziwekwe.**

Ili kuepuka mtego kwa wakurugenzi na wakuu wa wilaya, Babu ameagiza wawaelekeze wakandarasi au mafundi jamii (force account), kufunga taa ili kufanya kazi hiyo usiku na mchana.

Baada ya ukaguzi huo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Dk. Haji Mnasi, aliahidi kufuatilia mara kwa mara katika maeneo ya miradi ili kuhakikisha inakamilisha kwa wakati na wanafunzi wote kuingia darasani.



Katibu wa Jumuiya ya Wazazi wa CCM Kata ya Endiamtu, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Ernest Lukumay (kulia), akizungumza na watoto wa kituo cha Light In Africa kilichoko mji mdogo wa Mirerani baada ya kuwapa zawadi ya nguo na vyakula juzi. **PICHA: GIFT THADE**

# Wakulima wapewa somo mvua chache

**Na Cynthia Mwilolezi,** MANYARA

WAKULIMA mkoani hapa wametakiwa kutumia mvua zinazonyesha kupanda mazao yanayokomaa kwa muda mfupi kwa kutumia mvua chache zinazoendelea kunyesha nchini.

Kaimu Katibu Tawala wa Mkoa wa Manyara, Faraja Ngeragea alitoa rai hiyo juzi mjini Babati wakati akifungua Mkutano Mkuu wa 17 wa Mtandao wa Vikundi vya Wakulima na Wafugaji mkoani hapa (MVIWAMA).

Ngeragea, alisema mvua za mwanzo ni za kupandia, hivyo wakulima hao wanapaswa kupanda mbegu mapema mashambani ili wavune mazao miezi michache ijayo.

"Wakulima wa Manyara wanapaswa kutumia vizuri mvua hizi chache kupanda mbegu zinazoendana na msimu huu kabla mvua hazijaisha," alisisitiza.

Alipongeza juhudi za MVIWAMA kwa kusimamia wanachama zaidi ya 8,000 wa mkoa huo katika kilimo, ufugaji, mnyororo wa thamani wa nyuki, mbegu za asili na utunzaji wa mazingira.

"Kutokana na mabadiliko ya tabia nchi inabidi wakulima kujifunza mbinu za kilimo na ufugaji zinazokabiliana na mabadiliko haya tuliyonayo," alisema Ngeragea. Aliwahimiza wanachama wa MVIWAMA kutumia fursa zinazotolewa na serikali kuboresha kilimo na ufugaji na kunufaika kiuchumi.

Mratibu wa MVIWAMA, Valentine Ngorisa, alipongeza serikali za kupunguza tozo katika kilimo, kuboresha miundombinu, kuimarisha upatikanaji wa nishati mijini na vijijini na kuanzisha mfumo wa elimu bure.

"Kwa uhakika mfumo huo wa elimu bure utawawezesha watoto wa wakulima na watu wengine masikini kupata elimu ya msingi na sekondari na ni matumaini yetu kwamba hatimaye serikali itaweka mfumo kama huo katika ngazi ya chuo kikuu," alisema Ngorisa.

Aliipongeza serikali kwa kufuta umiliki wa ardhi, ambayo ilikuwa ikihodhiwa na wachache wakati wakulima walio wengi hawana ardhi ya kufanyia shughuli za kilimo na ufugaji.

"Tunamshukuru sana na kumuomba hatua hiyo ya Rais Samia Suluhu Hassan, iendelee bado kuna maeneo mengi ambayo yanahodhiwa na wachache huku wananchi wengi hawana ardhi kwa uzalishaji na wengine wakikodishwa ardhi yao wenyewe na wanaojiita wawekezaji.

Alisema bado kunasuasua katika kugawa ardhi iliyofutiwa umiliki wake, jambo linalokinzana na dhamira ya Rais Samia na kuleta malalamiko kwa jamii.

Alisema licha ya jitihada za serikali za kuimarisha sekta ya kilimo wakulima bado wanakabiliwa na changamoto nyingi za ardhi.

Alisema tatizo la wakulima wadogo na wanavijiji kunyang'anywa ardhi zao bado ni kubwa na migorogo mingine ni ya muda mrefu na ni vigumu kuelewa mpaka sasa haijapatiwa ufumbuzi.

Ngorisa, alisema bado kuna changamoto ya bei za mazao na soko la uhakika kwa mazao ya wakulima na mitaji na uwezeshaji wakulima.

"Tunaamini njia rafiki lazima zitafutwe ili vyombo vya kifedha na programu za uwezeshaji ziweze kuwafikia wakulima wadogo," alisema Ngorisa.

MVIWAMA ni jumuiya ya wanachama inayolenga kutetea maslahi ya wakulima, wazalishaji wa mazao ya mimea, mifugo na samaki wadogo.

Mkutano huo wa 17 umeshirikisha wanachama wawakilishi 128 kutoka Wilaya ya Babati, Simanjiro, Kiteto Hanang' na Mbulu.

# Ukatili watoto, wanawake wampasua kichwa mbunge

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MBUNGE wa Hai mkoani Kilimanjaro, Saashisha Mafuwe, amesema matukio ya ukatili wa kijinsia, ulawiti na ubakaji watoto na wanawake ni miongoni mwa mambo yanayompasua kichwa kwa sasa.

Aidha, alisema suala la wizi na ulevi uliokithiri kwa vijana katika Wilaya ya Hai, vimeathiri nguvu kazi ya taifa.

Mafue aliyaeleza hayo jana wakati wa sherehe za Maulid ya kuzaliwa Mtume Muhamedi (SAW) yaliyofanyika msikiti uliopo Mtaa wa Uzunguni Kata ya Bomang'ombe.

"Naombeni jambo moja, mashehe wangu mnafanya kazi ngumu, kumeibuka sasa hivi ukatili wa kijinsia, ubakaji na ulawiti, ulevi na wizi uliokithiri. Sasa tusaidiane kulinda nguvu kazi ya taifa ili tupate maendeleo na tulinde kizazi chetu," alisema Saashisha.

Mbunge huyo, amekumbusha Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, alipokuwa Hai kikazi, alivyokemea ulevi uliokithiri.

Mgeni rasmi katika Maulid hiyo, Shehe Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Shaaban Juma, aliwasihi viongozi wa dini kwa umoja wao kusaidiwa kuwekeza nguvu kukemea mambo hayo ili kizazi cha sasa kibaki salama.

Mwishoni mwa mwaka jana, Mchungaji Thomas Kudalisamu wa Usharika wa Ng'uni wa Doyasisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), akiwa kituo cha kulelea watoto yatima Lukani Children Center, alinukuliwa akisema kwa sasa kuna uuzaji pombe karibu kila nyumba Kijijii cha Ng'uni.

"Serikali ipo hakuna wa kudhibiti hili, kwa sababu hiyo vijana wengi wadogo wanajikuta wanakosa maadili, nguvu kazi ya taifa inapungua, muda wote vijana wamelewa," alisema.

Alisema ili kudhibiti hilo mapema ni lazima ifike mahali kanisa, serikali na wazazi kushirikiana.



## HABARI KANDA YA ZIWA

# Kutaka ubunge ni kosa, Maswi ahoji

**Na Ambrose Wantaigwa,**
TARIME

KATIBU Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Eliakim Maswi amehoji kuwa yeye kutaka ubunge ni kosa na kuonyesha kuwashangaa wanaosambaza taarifa hizo kwenye mitandao ya kijamii.

Maswi alihoji hivyo juzi, akilenga kuwajibu watu wakiwamo wanasiasa wanaosambaza taarifa kwenye mitandao hiyo kutokana na kuchangia miradi ya maendeleo wilayani hapa kuwa anafanya hivyo kwa lengo na kugombea ubunge katika Jimbo la Tarime Vijijini lililopo mkoani Mara katika Uchaguzi Mkuu utakafanyika mwaka huu kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Alisisitiza kuwa anaheshimu uamuzi wa wananchi na imani ya CCM kwa Mbunge wa sasa wa jimbo hilo, Mwita Waitara, hadi kipindi chake kitakapokamilika mwaka 2025 na kuwashangaa hao wanaofanya hivyo kwa nia ya kumchonganisha na kumkatisha tamaa kusaidia jamii.

**"Sijawahi kwenda kijijini, kitongoji au tawi lolote la chama, kutangaza ninataka ubunge, wamenitangaza wao, na nimefurahi kwamba kwa sasa najulikana jimbo zima,"**

"Sijawahi kwenda kijijini, kitongoji au tawi lolote la chama, kutangaza ninataka ubunge, wamenitangaza wao, na nimefurahi kwamba kwa sasa najulikana jimbo zima," alisema Maswi wakati wa hafla ya kukabidhi gari la wagonjwa katika Kituo cha Afya Kata ya Nyakonga wilayani hapa.

"Kama kuna msaada unahitajika nyumbani (Tarime) niko tayari kusaidia mara moja, lakini nikifanya hivyo baadhi ya watu wanasema ninataka ubunge, hivi mimi kutaka ubunge ni kosa? "alihoji kutokana na taarifa kusambaa katika mitandao kutoka kwa baadhi ya wanasiasa zikimhusisha na mbio za ubunge wa jimbo hilo.

Katibu wa CCM Wilaya ya Tarime, Noverty Kibaji, alisema wanachama wa chama hicho wanapaswa kuheshimu katiba kuepuka migogoro ya mara kwa mara inayosababisha makundi wakati wa uchaguzi.

Kibaji, alisema utaratibu wa mchakato wa kupata wagombea wa uongozi ndani ya chama hicho unafahamika kwa wanachama kuheshimiana na kuepuka kutangaza nia kabla ya kipindi cha ukomo wa madaraka wa wabunge na madiwani.

Chama hicho kilipata ushindi kiti cha ubunge wa jimbo hilo katika uchaguzi wa mwaka 2020 baada ya Waitara kumshinda John Heche wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) ambalo lilifahamika kama ngome ya upinzani tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa nchini.



Mbunge wa Lupembe wilayani Njombe, Edwin Swalle (aliyevaa kofia), akikabidhi gari la wagonjwa katika kituo cha afya Mtwango ambapo amesema litasaidia kuokoa maisha ya wananchi wa kata tano ikiwamo wanawake wajawazito na watoto. **PICHA: ELIZA KILINDI**

## Shule zagawawi miche ya miti

**Na Halima Ikunji,**
SIKONGE

HALMASHAURI ya Wilaya ya Sikonge mkoani Tabora imegawa zaidi ya miche ya miti ya matunda 1,000 kwa shule zake za msingi kusaidia kuboresha afya za wanafunzi na kuhifadhi mazingira.

Akizungumza wakati wa kugawa miche hiyo, Ofisa Umwagiliaji wa Halmashauri hiyo, Edgar Kasonga, alisema kila shule imepatiwa miche hiyo 45 ambayo itapandwa kipindi hiki ambacho mvua za masika zinanyesha nchini.

Kasonga, alitaja miche hiyo kuwa ni ya miembe, michungwa, mipera na mipapai.

"Mpande miti hii karibu na shule ili muweze kuifanyia ufuatiliaji wa karibu, msichague eneo lolote tu ili mradi ni eneo la shule. Mwakani, Idara ya Kilimo na Elimu tutakuja kukagua maendeleo ya miti mliyopanda," alisisitiza.

Mwalimu wa Shule ya Msingi Kipanga Mlimani, Petro Molgen, alisema endapo miti hiyo itastawi na kutoa matunda itachangia kuboresha afya za wanafunzi wao na kuwa bora na na makuzi mazuri.

Baadhi ya shule zilizokabidhiwa miche hiyo ni Chabutwa, Kabanga, Msuva, Ngoywa, Tutuo, Manyatwe, Usesula, Mpombwe, Jamhuri na Kipanga Mlimani.

# Wanafunzi hatarini kufa kwa ajali, ukatili

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

BAADHI ya wanafunzi wenye ulemavu wa Shule ya Msingi Jumuishi Buhangija ya Manispaa ya Shinyanga wako hatarini kufa kwa kugongwa na magari, kutoroka na kuvuka barabara kiholela kutokana na shule hiyo kukosa uzio.

Hayo yalisemwa juzi na Mwalimu Mkuu wa Shule hiyo, Fatuma Jilala wakati akipokea zawadi za Rais Samia Suluhu Hassan kwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Julius Mtatiro kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha kwa ajili ya wanafunzi hao kusherehekea Mwaka Mpya wa 2025. Fatuma, alisema wanafunzi hao wanaishi katika bweni la shule hiyo iliyopo pembezoni mwa barabara, wamekuwa wakitoroka mara kwa mara na wakati mwingine kwenda maeneo hatarishi bila wao kujua, ambako pia wanaweza kufanyiwa vitendo vya ukatili na udhalilishaji.

Alisema wanafunzi hao wenye ulemavu ukiwamo wa viungo, viziwi, bubu, wasioona na wenye ualbino wamekuwa wakitoroka na kuvuka barabara kutokana na kutokuwa na uwezo wa kutambua mwisho wa eneo la shule.

Akijibu ombi hilo, Mtatiro, alisema serikali itajitahidi kutatua changamoto hizo moja baada ya nyingine, huku akiwasihi walimu kuendelea kufundisha watoto hao kwa bidii ili wafaulu masomo yao na kutimiza ndoto zao.

Alisema Rais Samia ana upendo na watoto wenye uhitaji, na ndiyo maana amewapatia zawadi ya chakula kwa wanafunzi wanaioshi bweni kwa kuwa wameshindwa kujumuika na wazazi wao.

Alisema vilevile kiongozi huyo wa nchi, amekuwa akiboresha miundombinu rafiki kwao ya shuleni, ujenzi wa mabweni na kuajiri walimu wenye taaluma maalumu.

Kaimu Mkurugenzi wa Manispaa hiyo, Charles Luchagula, alitaja zawadi zilizotolewa kwa watoto hao kuwa ni mchele, unga wa ngano, sembe, sukari na mafuta ya kula.

Alisema vilevile ametoa taulo za kike katoni mbili, mafuta ya kupaka mwilini, chumvi, juisi na mbuzi aina ya beberu.

Kwa upande wao watoto hao, wamemshukuru Rais Samia kwa upendo na kuwapatia zawadi kwa ajili ya kufurahia sikukuu hiyo ya mwaka mpya wa 2025.

**ama**

**AFYA NA MAZINGIRA**

ALHAMISI JANUARI 2, 2025



Ukurasa 14

## PATA NJIA TANO ZA MAZOEZI YA MWILI YENYE UFANISI KIAFYA



## MGUNDUZI LULU HUNT... Mtaalamu lishe bora aliyevumbua kipimo kalori karne sasa imepita

Ukurasa 13

### ALIKOSIMAMA DK. SAMIA NA 2025 MPYA;

# Kamaliza mwaka, anaukaribisha mpya akimwangazia mama haki kiafya, hivi...

**Na Mwandishi Wetu**

Ni muda mrefu kumekuwapo kilio kinachoendana na walakini katika hali ya kinamama na mchakato mzima wa uzazi, hadi kupatikana mtoto.

Sura kuu ilijificha katika elimu au uelewa duni kuhusu suala hilo, kukosekana mahitaji muhimu katika nyumba za tiba, ngazi ya ujuzi na ushirikiano kijamii.

Kuna wakati katika Serikali ya Awamu ya Nne, kulikuwapo taasisi isiyo ya kiserikali chini ya Mama Salma Kikwete, ikajivisha sehemu ya wajibu huo, ikisambaza vitanda vya kusaidia huduma za uzazi.

Pia, ni katika awamu hiyo mapema, zikabuniwa mambo makuu mawili; Mpango wa Maendeleo ya Afya ya Msingi (MMAM) na sera yake mwaka 2007, ambazo maudhui yake yamekuwa na maana kubwa katika afya ya mama na mtoto hadi leo.

Mfumo wa kiserikali nchini, ikiwa na itifaiki ya kupokezana kijiti katika utendaji, ilipoingia madarakani Serikali ya Awamu ya Sita, nayo ikajikita kwa itifaki kuu mbili.

Mosi, kuendeleza ya MMAM na sera iliyoyakuta, pia kufanya ubunifu wake. Hapo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akawa na lake maalumu akiweka itikadi yake ya 'Mama Kashika Usukani' akizamia mapya yanayokomboa afua ya mwanamke kwa upekee.

Hapo akaanza na hatua kwamba, katika zaidi ya miaka mitatu ya uongozi wake, akaogeza bajeti maradufu, kwa sekta afya, mwanamama anufaike kwa kiasi kikubwa.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mohamed Mchengerwa, akidokeza Septemba mwaka huu kuwapo jumla ya hospitali za wilaya 129 zimejengwa nchini kote.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akizungumza jambo na Kareem Mjata, katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, jijini Dodoma, Februari mwaka huu. Rais akamhakikishia elimu yake, baada ya kupona. **PICHA: MTANDAO**

Takwimu za afya kitaifa, sasa zinaonyesha uwekezaji wa miundombinu ya afya; vituo vya huduma za afya kuongezeka kutoka 8,549 alipokuwa anaingia madarakani mwaka 2021 hadi 9,610 Machi mwaka jana; sawa na ongezeko la vituo 1,061.

Hapo ikivaliwa miwani, anaonekana mhitaji mwanamama, anapewa unafuu wa aiona yake.

**MANUFAA YAKE**

Hatua za manufaa yake inatajwa kwa mfano na Wizara ya Afya, Machi mwaka jana, kwamba kuna ongezeko la wajawazito waliojifungua kwenye vituo vya huduma za afya kutoka asilimia 63 mwaka 2021 hadi asilimia 85 mwaka mwaka 2023.

'Lengo la nchi ni kufikia asilimia 95 ya wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ifikapo mwaka 2030," anatamka wizara hiyo katika taarifa yake.

Pia, taarifa hiyo inadokeza kupunguzwa vifo vya wajawazito kwa asilimia 80, huku kukiimarshwa huduma za uzazi, mama na mtoto.

Mavuno yake hadi sasa ni kupunguzwa vifo vya wajawazito vitokanavyo na uzazi kutoka 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2016 hadi vifo 104.

Pia, inatajwa mageuzi hayo ya Rais Dk. Samia, ni kwamba vifo vya watoto wenye umri chini ya mwaka mmoja, vimepungua kutoka 43 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi 33 mwaka jana.

"Vifo vya watoto wachanga (wenye umri wa chini ya siku 28) vimepungua kutoka 25 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 hadi vifo 24 kwa vizazi hai 1,000 hadi sasa, " inaeleza taarifa hiyo ya Wizara ya Afya.

Eneo lingine la ufafanuzi wa wizara, ni kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano vifo vyao vimepungua kutoka 67 kwa kila vizazi hai 1,000 mwaka 2016 na kufika 43 mwaka 2022.

Hapo ndipo inapozaliwa swali la msingi, kuna hatua na mikakati ipi inayofanyika kufikisha mahali hapo?

**UMIRAISHAJI HUDUMA**

Wizara ya Afya katika taarifa yake in ufafanuzi kwamba, kati ya mwaka 2021 hadi Machi jana, Serikali ya Awamu ya Sita ikaendelea kuwekeza katika huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto, katika maendeleo kadhaa;

- Hapo kuna rekodi ya kukamilishwa ujenzi wa jengo kongwe la huduma za afya ya mama na mtoto, katika hospitali kongwe ya Meta, jijini Mbeya ikigharimu shilingi bilioni 13.2.
- Pia, kuna uendelezaji wa majengo ya Mama na Mtoto, kwenye hospitali za rufani za mikoa ambazo ni; Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe ambazo zimegharimu jumla ya shilin- gi bilioni 71.1.
- Kuna kuimarishwa huduma za upasuaji wa wajawazito kwa kuongeza, vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kwa mjamzito (CEMoNC) kutoka vituo 340 mwaka 2021 hadi kufikia vituo 523 mwaka 2023. Ni ziada ya 183.
- Kuanzisha wodi maalum kwa ajili ya huduma za watoto wachanga wagonjwa (Neonatal Care Units - NCU); hadi kufikia Desemba 2023, kuna jumla ya hospitali 189 zinatoa huduma za NCU ikilinganishwa na hyospitali 165 mwaka 2022 na Hospitali 14 tu mwaka 2018.
- Kumekuwapo uimarishaji, upatikanaji wa bidhaa za afya na uzazi, mama na mtoto, katika vituo vinavyomilikiwa na serikali, ukiongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 Za mwaka 2023.
- Kuimarishwa huduma za Saratani ya Mlango wa Kizazi; kukiwapo jumla ya mashine 140 za uchunguzi wa saratani zimenunuliwa na kusamba-

Inaendelea Uk. 12

AFYA

## 2025 NA DUNIA ILIKOFIKA...

# Umri wa mtu unavyogundulika kwa harufu, kila hatua inanukia kivyake



Picha zenye uwasilisho wa utashi wa mama na mwana, hali inayotajwa kitaalamu huendana na hisia za harufu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

Ni jambo la aina yake, hata ikirejewa katika tafakari ya kawaida tu, ikidodoswa kwa swali "Je, unaweza kujua umri wa mtu uliyekaa karibu naye kwa kunusa harufu ya mwili wake?

Mtu huyo anaweza kuwa hajajipuliza marashi, lakini unaweza kuujua umri wake kutokana na harufu ya mwili wake.

Bado kunatajwa, hakuna nadharia rasmi kuhusu hilo, lakini kuna utafiti unaothibitisha hayo kunusa 'harufu' ya mtu kubainisha umri wake.

Harufu ya mwili inatajwa kutofautiana kwa kila mtu, lakini hubadilika kadri anavyoendelea kuishi.

Ni mabadiliko ambayo mazingira anayoishi, bali hata mwelekeo wake kijamii na kimageuzi.

Wakati wa ututoni, inaelezwa kitaalamu, harufu ya mtoto huwa kidogo kutokana na tezi za jasho zisizo na shughuli nyingi, pia viumbe hai vidogo kwenye ngozi.

Hata hivyo, wazazi wengine wanatajwa wanaweza kugundua harufu ya watoto wao zaidi, kuliko watoto wa wenzao.

Harufu hiyo inatajwa kuunda uhusiano mzuri wa kihisia na kawaida, kati ya wazazi na watoto wao.

Pia, husaidia kupunguza msongo wa mawazo kwa wazazi, huku ikijenga hisia za furaha na upendo kwa mtoto.

Hapo kuna harufu maalumu inayotokana na watoto wanaokuwa, ikiwavutia zaidi.

Hata hivyo, inatajwa kinamama wanaosumbuliwa na hali ngumu kiafya baada ya kujifungua, kuna wakati hawawezi kunusa harufu ya mwili ya watoto wao.

### KUNUKIA MTOTO

Wakati wa umri wa kubalehe, harufu ya mwili ya mama hubadilika kila wakati.

Ni mabadiliko hayo yanayosababishwa na uzalishaji wa homoni za kijinsia, ambazo husisimua tezi za jasho na tezi za mafuta kwenye ngozi. Tezi nyingi za jasho huzalisha maji na chumvi.

Wakati tezi ziitwazo 'Aprokrini' huzalisha protini na mvuke unaohusiana na mafuta. Tezi hizo huzalisha harufu mbalimbali, ambazo ni za kipekee kwa kila mtu.

Pia, kinachoitwa 'Lipidi' na 'Sebum' ni kemikali ya mafuta inayolainisha nywele, ngozi na ngozi ya kichwa hutolewa kutoka kwa tezi hizo. Hata hivyo, ikichanganyika na bakteria, harufu ya miili ya binadamu huwa vibaya.



Hiyo ni sambamba na jasho la vijana, pamoja na harufu za miili yao, hubadilika na kutoa harufu mbaya.

Wanapofika umri wa kubalehe na kuingia utu uzima, harufu yao ya mwili inapungua na hivyo kupunguza uwezo wa wazazi kutambua watoto wao kwa harufu.

Kwa ujumla, kila mtu ana harufu maalum ya mwili, lakini inabadilika kadiri anavyokuwa.

### UTAJUAJE HARUFU YAKO?

Kuna swali, mtu atajuaje harufu yake? Hapo kuna maelezo kwamba utoaji mafuta katika tezi hizo, huongezeka wakati wa hatua ya kubalehe.

Ingawa nguvu zake hupungua mtu anapozeeka, kila mtu tayari anakuwa na harufu maalumu mwilini.

Hii inatajwa, kutegemea mambo mengi kama vile lishe, msongo wa mawazo, homoni, pia viumbe hai vya ngozi yake.

Uwezo wa mtu kunusa unatajwa kuwa mzuri sana katika kubaini habari kujihusu, hasa kiwa gizani au mazingira yaliyo na kelele, au wakati ambao ni vigumu kuona au kusikia kwa urahisi.

Harufu ya mwili husaidia katika kuchagua wapenzi, kutambua jamaa, au kutofautisha jinsia.

### HALI YA UZEENI

Mtu anapozeeka kitaalamu anaelezwa, ngozi yake hupoteza ubora na vimelea 'Kalojeni'. Hiyo inatajwa kupunguza shughuli za tezi za jasho na mafuta yake na kutokana na upungufu huo, inakuwa vigumu kwa wazee kudumisha joto la mwili.

Kuhusu tezi ziitwazo 'Sebasi', utoaji wao hupungua kadri mtu anavyozeeka; muundo wao pia hubadilika.

Ni hali inayosababisha kupungua kwa viwango vya Vitamini E au 'Squalene' ambavyo huzuia uzalishaji zaidi wa Oksijeni mwilini.

Ujumla wake unasababisha kuwapo harufu kwa wazee, ambayo Wajapani huita 'Kerisho'.

Hivyo, baada ya mtu kuwa na umri wa miaka 40, kazi ya baadhi ya tindikali za mafuta kwenye ngozi kama vile 'Omega 7' na 'Palmioleic' hubadilika. Hilo hubadilisha harufu ya mwili wa binadamu kwa ujumla.

***Kwa mujibu wa BBC. Soma zaidi, Uk. 14**

## KAMALIZA MWAKA, ANAUKARIBISHA MPYA AKIMWANGAZIA MAMA HAKI KIAFYA, HIVI...

**Inaendelea Uk. 14**

zwa kwenye vituo 140 vya kutoa huduma za afya katika halmashauri 104, katika mikoa 26. Vifaa vyote vina thamani ya shilingi bilioni 1.1.

- Mfumo wa M-mama; Serikali ya Rais Dk. Samia, imeanzisha mfumo wa kieletroniki unaoratibu rufani, kwa kusafirisha wajawazito na watoto wachan- ga wanaohitaji huduma za dharura.

Hiyo ni safari kutoka ngazi ya jamii hadi vituo vya kutoka huduma za afya au kutoka kituo cha ngazi ya chini, kwendangazi ya juu.

Kati ya mwaka 2022 hadi 2023, mfumo huo umeendelea kufanya kazi katika mikoa yote 31 ya Tanzania Bara na Zanzibar, kukiwapo wahusika 46,941 wamenufaika na huduma za dharura za rufani.

Wizara ya Afya kupitia ripoti yake mwaka jana, inatamka uwekezaji uliofanywa na Rais Dk. Samia Suluhu Hasssan, katika kuimarisha ubora wa huduma za afya ya Uzazi, Mama na Mtoto, viashiria vya nchi wanachama wa Shirika la Afya Duniani (WHO), Tanzania ikang'ara kufanya vizuri kuimarisha huduma za afya ya uzazi, mama na mtoto.

AFYA

### MGUNDUZI LULU HUNT...

# Mtaalamu lishe bora aliyevumbua kipimo Kalori karne sasa imepita

**Na Mwandishi Wetu**

- Kajipima, akajipunguza kibonge hadi 'kimodo'
- Alipoandikia kitabu, ukageuka mtindo maisha
- Wanasayansi wakageuza kipimo cha utapiamlo

IDADI ya kalori huonekana kwenye lebo nyingi za vyakula na vinywaji vilivyopakuliwa na hata kwenye menyu za baadhi ya migahawa. Taarifa hizo zinapatikana kwingi.

Dunia iliyopiga hatua kiteknolojia, mtu anaweza kujua hatua za kutembea, akachoma kalori zake kila siku kwa kutazama kipimo kwenye simu yake.

Pia, kwenye ukumbi wa michezo ya mazoezi ya viungo, pia kunatajwa kuwapo vielelezo vya kalori.

Msingi wake kalori, ni neno la Kilatini "calor" linalomaanisha 'joto.' Liligunduliwa kwa mara ya kwanza na mtaalamu Mfaransa wa Kemia na Fizikia, Nicolas Clément katika miaka 1820.

Kalori ilikuwa kipimo cha joto kinachoweza kubadilishwa kuwa nishati, na kilitumika kupima kiasi cha mvuke kuendesha injini za mitambo.

Suala la kuhesabu kalori ilikuwa jambo geni karne moja iliyopita. Nafasi yake kuwa kipimo cha lishe, ilianza kutumika mwishoni mwa Karne ya 19.

Hapo ndipo miaka 1920, mtaalamu Lulu Hunt Peters, daktari wa Kinarekani, mhitimu wa Chuo Kikuu cha California, akafanya mageuzi kuja na mahesabu ya kalori.

Ghafla akawa wa kipekee, maana wakati huo wanawake walikuwa chini ya asilimia tano ya wanafunzi wanaosomea udaktari nchini Marekani.

Ingawa sasa kalori zinajulikana kwa kuhesabu, tafiti zinaonyesha kwamba karibu asilimia 80 ya watu wanaopunguza uzito mkubwa kwa kupunguza ulaji wa kalori, wanarudi tena kwenye uzito wao wa awali.



Dk. Lulu Hunt Petersi, katika umbile jipya. **PICHA: MTANDAO.**

**KIPIMO CHA CHAKULA**

Maana ya leo ya kalori ya sasa (joto linalohitajika kuinua kilo moja ya maji kutoka nyuzi joto 0 hadi 1° Celsius) iliingia kwenye uwanja wa lishe ya binadamu, kutokana na kazi ya mtaalamu wa kemia, Mmarekani, Wilbur O. Atwater.

Atwater alichukua likizo ya mwaka mmoja kwenda Ujerumani, alikojifunza kutumia kipima joto kinachoitwa Kalorimeter, kifaa kinachotumika kupima kiasi cha joto kinachotolewa au kupokewa na miili.

Wakulima wa Kijerumani walikitumia kuzalisha chakula bora kwa mifugo yao.

"Aliporejea kwenye maabara yake huko Connecticut, Atwater alijaribu kurudia mchakato huu, si kwa ajili ya lishe ya mifugo, bali kwa ajili ya chakula cha binadamu," anaeleza Profesa Giles Yeo, mtaalamu wa Niurolojia (neuroendocrinology) katika Chuo Kikuu cha Cambridge, Uingereza.

Hapo akaanza kuchapisha majarida yenye maelezo ya kina kuhusu kalori o katika vyakula, kiasi kinatoka kwenye lishe za; protini, mafuta na kabohaidreti.

Kwa sasa inaonekana jambo lililozoeleka kufahamu tufaha lina kalori kidogo ukilinganisha na donati haikuwa imejulikana miaka 100 iliyopita

"Kanuni maarufu inayofundishwa shuleni (kalori 4 kwa gram 1 ya protini, kalori 4 kwa gram 1 ya kabohaidreti, na kalori 9 kwa gram 1 ya mafuta), anasema mtaalamu Yeo,

**ZAMA UTAPIAMLO**

Wakati utapiamlo ulikuwa tatizo, taarifa hizo zilikuwa muhimu kusaidia jamii maskini kula vizuri kwa rasilimali chache walizo nazo.

"Awali, watu walijali zaidi ni kalori ngapi wataweza kupata kwa bei rahisi," anasema Helen Zoe Veit, mtaalamu wa historia ya chakula katika Chuo Kikuu cha Jimbo la Michigan, Marekani.

"Hata waajiri wengine walitumia kalori kuthibitisha malipo ya chini, wakisema, 'kulingana na hesabu ya kalori, unapaswa kuwa na uwezo wa kununua chakula cha kutosha kwa kile tunachokulipa,'" anasema pia mtaalamu huyu wa historia ya chakula.

**MABADILIKO KIJAMII**

Mwanzoni mwa karne ya 20, wakati upatikanaji chakula uliongezeka na maendeleo ya teknolojia mpya za kuhifadhi na kusafirisha chakula, idadi ya watu, hasa nchini Marekani ilianza kuongezeka.

Akiwa ameelewa kazi za Atwater kupitia taaluma yake, daktari huyo alikuja na wazo la kutumia zana zilezil, kuhesabu kalori, katika kampeni za kupunguza kilo alizoziona tatizo.

Akatumia mantiki ya kimaandishi (kula kidogo kuliko unavyotumia), Lulu, ambaye wakati huo alikuwa na uzito wa karibu kilo 90, alifanikiwa kupunguza karibu 30.

Akafurahishwa na matokeo hayo na akaanza kuandika kila mara matokeo yake kwenye safu ya makala katika magazeti ya wakati huo, akielezea mbinu yake yaa kupunguza, hatimaye akaandika kitabu chake.

Hapo mitindo pia ilibadilika, kulingana na dhana mpya ya uzuri inayohimiza mwili wenye umbo uliochongeka. Mtindo mwingine uliipatia umaarufu wakati huo, ni kuwa kama vile mkanda wa kiunoni ulioanza kupitwa na wakati.

Mafanikio ya Lulu katika kubadilisha mwili wake kuwa unaohamasisha, kitabu chake kikawavutia hasa wanawake (weupe na tabaka la kati).

"Ni kitabu kilichoandikwa vizuri," anasema Profesa Yeo, ingawa leo maoni yake yangetafsiriwa kama ubaguzi dhidi ya watu wanene, maandiko yake ni ya kufurahisha na ya kuvutia," anasema.

Mwamdishi mwenyewe alikuwa na uzito wa ziada, hivyo maoni yake wakati huo yalionekana ya kujikosoa, badala ya kumshtumu mtu kuwa "mnene kupita kiasi".

**UZITO NA AFYA**

Lakini kitabu hicho kilikuwa na athari kubwa kwa sababu kuna wakati, maono mapya ya mwili yalikuwa yakijitokeza, pia kwa sababu uhusiano kati ya mafuta ya ziada mwilini na afya ulianza kugunduliwa.

"Katika miaka ya 1910, ushahidi mpya ulionyesha kuwa uzito kupita kiasi unaweza kuwa na madhara," anasema Veit.

"Tafiti zilizofanywa na makampuni ya bima, kwa mfano, zilionyesha kuwa kadri watu wanavyokuwa na uzito mkubwa baada ya umri wa miaka 35, ndivyo walivyokuwa na uwezekano mkubwa wa kufariki," anafafanua

Ingawa mapendekezo ya Peter yaliangazia kalori 22, akielewa kuwa unapaswa kula kwa kiwango hitajika na kula lishe bora, lakini hakukataza kabohaidreti, nyama na maziwa.

Mtaalamu Profesda Yeo, anaelezea kwamba, mti akilinganisha miiko kupunguza unene kupita kiasi, kama vile matumizi ya aina fulani za dawa za kulevya; uvutaji sigara na matumizi ya mipira. Mkakati wa mtaalamu Peter, haukuwa na ishara kuwa haufuati maagizo ya kiafya.

**MATUMIZI YA KALORI**

Kuzingatia habari mpya kuhusu lishe, muundo wa chakula, mwili wa binadamu unavyofanya kazi, tunafahamu njia ya bora ya kuhesabu kalori, huku tykudumisha lishe bora au hata kupoteza uzito kwa njia endelevu.

Bado, hamu ya kuhesabu haijaisha kabisa katika mtindo na wengi wanaamini kuwa, mawazo hayo yanachangia kukabili shida iliyoko katika jamii ya unene kupita kiasi.

Ingawa kalori hazina maana ya moja kwa moja afya ya mtu, lakini bado ina matokeo katika maisha, Profesa Yeo, akiwa na ufafanuzi: "Ni njia rahisi ya kufanya maamuzi, lakini inamaanisha kuzingatia jambo lisilofaa."

- ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***

AFYA

# PATA NJIA TANO ZA MAZOEZI YA MWILI YENYE UFANISI KIAFYA

**Na Mwandishi Wetu**

MAZOEZI ya mwili, sio lazima kiafya yanatajwa yawe magumu. Hata kutembea haraka kwa dakika 10 kwa siku, kunatajwa kuwa na manufaa mbalimbali ya afya.

Inatajwa kupunguza hatari ya magonjwa mbalimbali, ikiwamo ya moyo, kiharusi na baadhi ya kisaratani.

Inatajwa kitaalamu kwamba, mabadiliko machache kwenye jinsi mtu anavyotembea, yanaweza kubadilisha mazoezi hayo kuwa rahisi na yakifanyika kila siku, kwa manufaa zaidi kwa afya ya mtembeaji.

Ikiwa mtu anapenda kupata faida zaidi kiafya, kutokana na matembezi yako, hapo kuna njia tano za kuyafanya kuwa ya manufaa zaidi:

Mosi, tofautisha kasi: Njia mojawapo inayoongeza faida za kutembea ni kubadilisha kasi ya kutembea, badala ya kudumu katika mwendo uleule.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mama Mariam Mwinyi (katikati), aliposhiriki mazoezi ya viungo, baada ya kutembea kuanzia Barabara ya Ofisi ya Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) Mazizini hadi Uwanja wa Amaan, Unguja. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

Pia, mtu anatakiwa kujumuisha vipindi vya kutembea haraka, ikifuatiwa na polepole.

Mbinu hiyo inajulikana kama kutembea kubadilisha kasi kwa vipindi, kwamba kunaboresha utendaji wa moyo na mishipa yake kwa ufanisi zaidi, kuliko kutembea kwa kasi isiyobadilika.

Utafiti uliofanywa kwa miezi minne, kupishana kwa dakika tatu za kutembea haraka na dakika tatu za kutembea kwa mwendo wa wastani, kulionyesha maboresho makubwa zaidi katika udhibiti wa sukari ya damu na viwango sawa vya mwili.

Hiyo inatajawa ni kwa watu wazima walio na ugonjwa wa kisukari cha aina ya pili, kuliko waliotembea kwa miguu kila mara, wakiwa na kasi sawa.

Kutembea kwa muda, pia husababisha kupunguzwa mafuta mwilini na kunaboresha ukakamavu, pia ustahimilivu wa jumla mwilini.

Ili kujumuisha hili katika matembezi yako ya kila siku, mhusika anashauri ajaribu kuongeza mwendo wako kwa dakika chache, kisha anarudi kwenye kasi yake ya kawaida.

Ni jambo linalofanyika kwa kurudia mzunguko huo wa matembezi, ili kuongeza mapigo ya moyo na kuchoma kalori zaidi.

Pili, tembea kwa mwendo kasi, kutembea haraka sio tu ya kunakufikisha unakoenda mapema, pia ni njia inayoleta faida zaidi kiafya.

Takwimu zilizochambuliwa kwa zaidi ya watu 50,000 wanaotembea, iligundulika kuwa mwendo wa angalau maili tatu kwa saa, ulihusishwa na kupunguza hatari ya kifo kutokana na sababu kadhaa

Hapo imajumuisha hatari ya chini ya kifo kutokana na ugonjwa wa moyo na mishipa, pia maradhi ya saratani.

Watafiti pia, wameonyesha kwamba, kuongeza kasi ya kutembea, kunaweza kuboresha afya ya moyo ya mtu na kusaidia kudhibiti wa uzito.

Mtu anatajwa akiwa hana uhakika kuhusu mwendo wako, ajaribu kutembea kwa kasi ambapo unapumua haraka zaidi, lakini bado anaweza kufanya mazungumzo.

Tatu, kuongeza uzito wa kubeba: Mtu anapobeba mzigo au uzani wa ziada wakati wa kutembea, kunaweza kumwongezea nguvu ya mazoezi.

Kwa kuvaa fulana au mkoba wenye uzani, kunalazimisha misuli yako kufanya kazi kwa bidii zaidi - kuongeza nguvu na kuchoma kalori zaidi.

Inatajwa, mtu anapotaka kujaribu, ni muhimu akaanza na uzito mdogo, ili kuepuka matatizo au majeraha.

Tafsiri ya uzani huo, unaanzia kwenye mavazi kama fulana au mkoba, unaowakilisha asilimia tano ya uzito wa mwili wake.

Mtu mwenye uzani wastani kwa mfano kilo 80, anaweza kuanza kwa kuongeza kilo nne pelee, ukiwa uzani wa ziada kwenye mkoba wake.

Kwa hatua, akaongeza kiwango cha uzito unaobeba kadiri unavyojisikia vizuri zaidi na ahakikishe uzito unabebwa, unasambazwa sawa, ukidumisha mkao mzuri wakati mtu anatembea (usielemee, ukande mmoja).

Nne, safari ipitie milima au ngazi: Kuchagua mwelekeo unaofaa kwenye matembezi, kunasaidia kuleta mabadiliko makubwa safarini.

Matembezi kwenye milima au ngazi, kunashirikisha sehemu tofauti ya misuli, hasa miguuni, ikilinganisha kutembea kwenye ardhi tambarare.

Hii sio tu huongeza nguvu, pia anachoma kalori zaidi, kwani kutembea kwa miguu na huongeza kasi ya mazoezi yake, bila kuhitaji kutembea haraka.

Zaidi ya hayo, huwa anatembea chini, pia inaboresha kazi ya misuli na uthabiti wa mwili wako.

Tano, inatajwa haja ya mtu kujizoesha kutembea kwa uangalifu. Jinsi ya kuanza hapo, napo panaelezwa kutembea hakuishii kw manufaa ya kimwilini, pia kunaweza kuboresha ustawi wako wa akili wa mtu.

Tafsiri inayotolewa ni kwamba, kunahusisha kuzingatia kwa makini mwenendo, kupumua na mazingira yaliyoko.

Inarajewa kuwapo utafiti unaoonyesha kuwa watu waliofanya mazoezi ya kutembea kwa uangalifu kila mara, kwa walau mwezi mmoja.

Hapo walishuhudia kupunguza viwango vya mfadhaiko na maboresho kwa afya yao ya akili kwa ujumla.

Mtu anashauriwa kutembea kwa uangalifu, akianza kwa kuzingatia hisia za kila hatua, mdundo wa anavyopumua, pia sauti zinazokuzunguka.

Inatajwa kuboresha afya ya akili, huku matembezi yakifanywa kuwa ya kufurahisha zaidi na kinachifuata zaidi ni; kuongeza mielekeo kwenye matembezi, kwa dhumuni ya kuleta mabadiliko makubwa.

**NAMNA KUANZA MAZOEZI**

Jinsi ya kuanza: Inatajwa suala la kuboresha matembezi yako hakuhitaji mabadiliko makubwa, lakini kuna mambo machache unapaswa kukumbuka ili kukaa salama, kupunguza hatari yako ya kuumia, na kuongeza manufaa:

Pasha joto na punguza mwendo: Anza na dakika chache za kutembea kwa urahisi ili kupasha misuli joto. Maliza matembezi hayo kwa kupunguza mwendo na umalize kwa kunyoosha taratibu ili kuupoza mwili wako.

Vaa viatu vinavyofaa: Chagua viatu vizuri na usaidizi mzuri ili kuepuka majeraha.

Tembea na maji: Lete maji, haswa unapotembea kwa muda mrefu au katika hali ya hewa ya joto, ili kuzuia upungufu wa maji mwilini.

Sikiliza mwili wako: ikiwa unahisi maumivu au usumbufu, punguza kasi au pumzika. Ongea na daktari wako ikiwa shida inaendelea.

Hatua kwa hatua ongeza kiwango: Ikiwa unaongeza uzito, kukabili vilima, au kuongeza kasi, fanya hivyo hatua kwa hatua ili kuruhusu mwili wako kubadilika.

Hiyi inamaanisha kufanya mazoezi ya ziada kidogo kila wakati, ili kutathmini jinsi mti anaavyohisi.

Kwa ujumla, kunaelezwa kutembea ni njia nzuri ya kuboresha na kudumisha afya ya mwili, hatua inayoenda na kufanyika marekebisho madogo kwenye mwendo huo

Hilo lifanyika, ndani ya tabia ya utembeaji wa kila siku, huku kisakilijia ikiwa ni njia ya bora na inayofurahisha.

• ***Kwa mujibu wa taarifa za kimataifa.***



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipokuwa Makamu wa Rais mnamo Agosti 2020, aliposhiriki matembezi ya kilomita nne yaliyoanzia kwenye makazi yake Mtaa wa Farahani Kilimani jijini Dodoma, akihitimisha kwa kuwasisitiza Watanzania kuzingatia mazoezi ya mwili.





# Wataalamu Naliendele wapiga kambi Singida

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Naliendele mkoani Mtwara imeanza kutoa mafunzo kwa wakulima na maofisa ugani wa Halmashauri ya Wilaya ya Singida ya kilimo cha korosho kwa lengo la kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini.

Mafunzo hayo yalianza kutolewa juzi kwa wakulima hao 30 na maofisa hao 15 katika shamba la mkulima Mustapha Mwangi lililopo Kata ya Ilongero kwa lengo la kupunguza athari za wadudu na magonjwa yanayoweza kupunguza uzalishaji na tija ya zao hilo.

Mtafiti kutoka TARI, Gasper Mgimiloko, alisema wameanza kutoa mafunzo hayo kwa wakulima ili waweze kutambua umuhimu wa matumizi sahihi na salama ya viwatilifu na kudhibiti visumbufu vya korosho.

Alitaja mafunzo wanayopatiwa kuwa ni namna ya upuliziaji wa viwatilifu, matumizi ya mavazi kinga, mbegu bora, utunzaji wa shamba, uchanganyaji wa mazao na upogoleaji.

Mgimiloko, alisema mafunzo hayo ni muhimu pia kwa maofisa ugani, hasa wale waajiriwa wapya ili kuongeza uelewa wao kuhusu uzalishaji wa korosho, hususan wanatoka maeneo ambayo hayana uzoefu na zao hilo.

**"Lengo la kuwajumuisha maofisa ugani tunaamini tayari wana mafunzo walioyapata vyuoni, lakini kuna ambao ni waajiriwa wapya yamkini wanatoka sehemu au kanda...**

"Lengo la kuwajumuisha maofisa ugani tunaamini tayari wana mafunzo walioyapata vyuoni, lakini kuna ambao ni waajiriwa wapya yamkini wanatoka sehemu au kanda ambazo hazilimi korosho kwa hiyo lengo pia ni kuwaongezea wigo wa uelewa juu ya uzalishaji wa zao hili," alisema.

Ofisa Ugani Mifugo Kata ya Kinyagigi, Valeth Nyamwonyo, aliishukuru TARI kwa mafunzo hayo ambayo yatawawezesha wakulima kupata ujuzi wa namna bora ya uzalishaji wa korosho.

Mkulima, Emiliana Lisu kutoka kata ya Kinyagigi, ameahidi kuyafanyia kazi mafunzo aliyoyapata.

"Mafunzo haya yamenisaidia kama mkulima wa korosho kufahamu namna bora ya kulima zao hili na pia nimefahamu udongo unaofaa kwa kuotesha mikorosho na matumizi sahihi ya viwatilifu," alisema.

Mmiliki wa shamba lililotumika kwa mafunzo hayo, Mustapha Mwangi, alieleza namna yalivyomsaidia kufahamu thamani ya kilimo cha korosho na kuboresha shamba lake ambalo hapo awali halikutoa mavuno mazuri.

"Nimefaidika na mafunzo haya kwa sababu mambo mengi tulikuwa tunasoma kwenye makaratasi na vitabu ila tunashindwa tuyafanyaje," alisema.

Ekari 268 hutumiwa na wakulima katika Halmashauri ya Wilaya ya Singida kulima korosho.



Askofu Mkuu wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God Tanzania, Dk. Evance Chande (kushoto), akiwaombea watoto wanaosoma shule kwenye ibada ya shukrani kwa kufika mwaka mpya wa 2925 iliyofanyika Ipagala Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wahamasishwa kuchangamkia miradi ya serikali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAKAZI mkoani hapa, wametakiwa kuchangamkia fursa ya miradi inayotekelezwa na serikali kujikwamua kiuchumi kwa kipindi cha mwaka huu.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary

Senyemula, wakati akizungumza na waumini madhehebu ya dini kwenye ibada ya mkesha wa kitaifa wa dua maalum uliofanyika jijini hapa.

Mkuu huyo wa Mkoa wa Dodoma akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan kwenye ibada hiyo, aliwataka wakazi hao kuzitumia fursa zilizopo na zijazo kujiinua kiuchumi na kukabiliana na hali ya ngumu ya maisha.

"Uwekezaji uliopo kupitia miundombinu mbalimbali inawawezesha kwa mtu mmoja mmoja kujipatia fedha ikiwa mtaanzisha biashara, kufanya kazi kwenye miradi hiyo kwa hivyo niwaombe mjitokeze kuchangamkia fursa hizo zilizopo," alisema.

Aliwakumbusha kuhakikisha mwaka huu wanamuomba Mungu Uchaguzi Mkuu ufanyike kwa amani na haki na kupata viongozi wa kuwatumikia Watanzania bila kujali itikadi zao.

Mwaka huu nchini kutafanyika uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani nchini ambao kwa mujibu wa Katiba utafanyika kila baada ya miaka mitano, ukivishirikisha vyama vingi vya siasa.

Mwenyekiti wa mkesha huo, Askofu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Fellowship of Churchs (TFC), Dk. Godfrey Malasi alisema lengo ni kutoa shukrani ya kitaifa kwa mwaka uliopita na kuomba baraka kwa mwaka mpya wa 2025.

"Lengo lingine ni kuwahamasisha Watanzania kushirikiana kwa pamoja kuombea uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka huu, maendeleo ya kiroho, kijamii na kiuchumi kwa Taifa letu na kuthibitisha mshikamano wetu kama Taifa linalongozwa na amani na utulivu endelevu," alisema Askofu Dk. Malasi.

# Viongozi IRDP wapigwa msasa

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

VIONGOZI watendaji wa Taasisi ya Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) wamepata mafunzo ya kuboresha utendaji kazi wao.

Mafunzo hayo ya siku tatu yalitolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC) jijini hapa.

Akizungumza wakati wa kufungwa kwa mafunzo hayo jana jijini hapa, Mkuu wa IRDP, Profesa Hozen Mayaya alisema ni muhimu kusaidia kukuza weledi miongoni mwa viongozi wa chuo hicho.

Alitaja baadhi ya mada zilizotolewa katika mafunzo hayo kuwa ni uadilifu na uongozi, nidhamu ya uongozi, mawasiliano kazini na itifaki na ustaarabu.

Mengine ni kuwa na akili ya kihisia, ujuzi muhimu ambao unahitaji kukumbatiwa na viongozi na wafanyakazi katika taasisi zote.

# TAKUKURU 'yafumua' mifumo kuboresha huduma

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma imesema imefanya uchambuzi wa mifumo 11 kwa ajili ya kuboresha utendaji kazi za serikali na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mkuu wa TAKUKURU wa mkoa huo, Victor Swella, alisema taasisi hiyo imefanya chambuzi hizo ili kuhakikisha mifumo hiyo haikwamishi jamii kupata huduma kutoka mamlaka husika mkoani hapa.

Swella, aliitaja mifumo iliyofanyiwa chambuzi kuwa ni pamoja wa udhibiti wa mapato ya uvuvi katika Wilaya ya Bahi, wa usimamizi wa mawasiliano na utunzaji wa nyaraka na kumbukumbu (Mpwapwa) na wa usimamizi na uendeshaji wa biashara ya nyama (Kondoa).

Aliitaja mifumo mingine kuwa ni ushiriki wa wananchi katika miradi ya maendeleo, uagizaji, upokeaji na usambazaji wa vifaa tiba katika Halmashauri ya Kondoa, wa mianya ya rushwa katika mchakato wa uunganishwaji wa umeme kwa wananchi Wilaya ya Bahi na wa msamaha wa matibabu kwa wazee na makundi maalum katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

"Tunafanya hizi chambuzi ili kubaini kama zina changamoto ziweze kufanyiwa marekebisho kuondoa usumbufu kwa jamii inayojitokeza kupata huduma kupitia mifumo hiyo," alisema Swella.

Mingine iliyofanyiwa uchambuzi ni ule wa mianya ya rushwa katika usimamizi wa fedha za serikali za mitaa Halmashauri ya Chamwino, wa usimamizi wa fedha za michango ya wananchi katika vijiji vya Wilaya ya Chemba.

Vilevile, alisema taasisi hiyo imeendelea na utoaji elimu kwa jamii ya kupiga vita rushwa katika maeneo mbalimbali kwa kutumia njia tofauti ili kufikisha ujumbe kwa wananchi.

Alisema wamekuwa wakitumia mikutano ya hadhara, makongamano na kuandaa michezo na kufikisha urahisi ujumbe kwa rika tofauti.

Alisema pia wamekuwa wakitoa elimu ya kupiga vita rushwa katika shule za msingi, sekondari na vyuo kwa kuanzisha klabu za kupinga rushwa na kusaidia kuelimisha jamii.

Swella, alisema klabu hizo zimekuwa mabalozi wazuri wa kuelimisha jamii kuhusu madhara ya kutoa na kupokea rushwa.

Swella, alifafanua kuwa lengo ni kuisogeza jamii karibu na taasisi hiyo kwa ajili ya mapambano dhidi ya rushwa kwa kuwa ni jukumu la kila mmoja.



# Wananchi waja juu, waomba wawekezaji waondolewe

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WAKAZI wa Kata ya Ifumbo Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, wameiomba serikali kuwaondoa wawekezaji kwa madai ya kuvamia Mto Zira, kuchimba dhahabu na kuharibu mazingira.

Wakazi hao walidai kuwa wameiomba serikali kufanya hivyo baada ya jitihada zao za kuwazuia ili kulinda mazingira ya mto huo kugonga mwamba kutoka na kuambulia vipigo kutoka kwa wawekezaji hao, kupora pikipiki na kutishiwa kubambikiwa kesi na kufikishwa mahakamani.

Walida kuwa shughuli hizo ni ukiukwaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan aliyoyatoa wilayani hapa akiwa Makamu wa Rais ya kupiga marufuku uchimbaji kufanyika kwenye mito miwili ukiwemo huo wa Zira na Lupa.

Wakazi hao walitoa madai hayo juzi wakati wa ziara ya Waziri wa Madini, Anthony Mavunde katika kata hiyo ya kukagua shughuli za uchimbaji zinazofanyika eneo hilo na utekelezaji wa sheria za nchi.

Mmoja wa wakazi hao, Abel Mlangali, alisema Rais Samia alipiga marufuku shughuli hizo kwa lengo la kulinda Ziwa Rukwa ambalo mito hiyo inamwaga maji ili kudhibiti kuongezeka kina kutokana na kujaa mchanga na tope.

Mlagali, alidai pamoja na marufuku hiyo, baadhi ya wachimbaji wakiwemo wawekezaji wanaendelea na shughuli zao ndani ya mto huo kwa kutumia mitambo ya kisasa na kuharibu mazingira kwa kiwango kikubwa.

Alidai wakazi hao wametumia mbinu mbalimbali kudhibiti uharibifu huo, lakini unaendelea huku baadhi ya wawekezaji hao wakiwashambulia kwa vipigo na kuwapora vyombo vyao vya usafiri hasa pikipiki.

**“Ili shughuli za uchimbaji zianze ni lazima kuwepo na leseni na mmiliki wa leseni apate cheti cha Tathimini ya Athari za Mazingira (EIA) ambacho kinatolewa na NEMC, sasa hapa siwezi ...**

“Tumekuwa tukitekeleza agizo la rais kwa kuulinda huu mto, lakini tunapigwa mabomu na kupora pikipiki zetu, sasa tunaomba mtusaidie mto wetu uendelee kuwa salama, asiwepo mwekezaji wala wachimbaji wazawa, wote waondolewe,” aliendelea kudai Mlangali.

Alidai mto huo wameulinda kwa muda mrefu kwa sababu wanaoutegemea kwa shughuli mbalimbali, lakini kwa sasa uharibifu umekuwa wa hali ya juu. Michael Sanga, alidai baadhi ya wachimbaji wana leseni na vibali kutoka serikalini hali ambayo inaashiria kuwepo kwa hujuma za makusudi za baadhi ya maofisa wake.

Sanga, aliomba leseni hizo zifutwe ili mto huo uendelee kuwa salama na sheria za nchi kuzingatiwa na kila mdau wa maendeleo ili kuhakikisha mazingira ya mto huo yanakuwa salama. Alidai kitendo cha wao kupigwa mabomu ya machozi wakati hawana silaha ni kosa kwa mujibu wa sheria na kuiomba serikali iwalinde.

Diwani wa Kata ya Ifumbo, Weston Mpyela, alisema kutokana na kusimamia mto huo usiharibiwe, wamekuwa wakipokea vitisho kutoka kwa baadhi ya wawekezaji hao kukamatwa na kuwapeleka mahakamani kwa tuhuma ambazo hazieleweki.

Mpyela, alisisitiza pamoja na vitisho hivyo, wataendelea kuulinda mto huo na kuhakikisha unaendelea kuwa salama kwa maendeleo yao na vizazi vijavyo. “Tunaomba vyombo vya dola viendelee kuchunguza jambo hili kwa sababu tunapata vitisho vingi, sisi tuko tayari kupelekwa mahakamani kwa sababu ya kuendelea kuulinda mto wetu,” alisemaa.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alithibitisha uharibifu wa mazingira kufanyika kwa kiwango kikubwa katika eneo hilo.

Homera, alisema uharibifu huo haujafanywa na mwekezaji pekee pia na baadhi ya wakazi wa eneo hilo. Alisema hajawahi kufika katika eneo hilo bali aliwahi kuongozana na aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Seleman Jaffo na Maofisa wa Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC) katika eneo la jirani na kushuhudia uharibifu.



Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (mwenye kofia nyeusi), akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, pamoja baadhi ya viongozi wa Serikali wa Wilaya ya Chunya hivi karibuni kukagua eneo la Mto Zira katika Kata ya Ifumbo wilayani Chunya ambalo limeharibiwa kutokana na shughuli za uchimbaji wa Madini ya dhahabu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Igoma wawezeshwa kuezeka kituo cha polisi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAKALA wa Huduma za Misitu nchini (TFS) umetoa msaada wa mabati 96 kwa ajili ya kuezeka Kituo cha Polisi cha Igoma mkoani hapa baada ya kujengwa kwa nguvu za wananchi.

Msaada huo ulitolewa juzi kupitia Shamba la Miti la Kiwira, ikiwa ni mchango TFS kwa jamii inayozunguka shamba hilo kutambua ushiriki katika uhifadhi wa misitu na shamba hilo.

Akikabidhi mabati hayo kwa Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Beno Malisa, Mhifadhi Mkuu wa shamba hilo, Thadeus Shirima, alisema uongozi wa TFS umeamua kutoa msaada huo kuunga mkono jitihada za wakazi wa Kata ya Igoma kujenga kituo hicho kwa nguvi zao.

Shirima, alisema kituo hicho kipo jirani na shamba hilo, hivyo na wao kama sehemu ya jamii wameamua kushiriki katika ujenzi huo kwa kutoa mchango huo wa mabati.

“Wananchi wanaoishi kuzunguka shamba letu ni watu ambao tunashirikiana katika ulinzi wa misitu na rasilimali nyingine zilizo ndani ya shamba hili, hivyo kwa kutambua mchango wao tumeamua kuwaunga mkono katika ujenzi wa Kituo cha Polisi,” alisema Shirima na kuongeza

“Hata sisi kama sehemu ya jamii tunaamini pia tutanufaika na uwepo wa kituo hiki, hivyo nasi tumejisikia kutoa mchango wetu kama wanufaika.”

Akizungumza baada ya kupokea mabati hayo, Malisa, alisema kukamilika kwa kituo hicho kutasaidia kuimarisha ulinzai wa wakazi hao na kata jirani ambako kuna idadi kubwa ya watu na shughuli nyingi za kiuchumi.

“Wananchi wa eneo hili ni wakulima wazuri wa viazi mviringo na mazao mengine ya kibiashara, pia kuna shamba la miti la Serikali na ya watu binafisi,” alisema na kuongeza:

“Kutokana na shughuli hizi za kiuchumi eneo hili lina mwingiliano mkubwa wa watu hali ambayo inasababisha kuwepo kwa uhitaji mkubwa wa Kituo cha Polisi kwa ajili ya kuimarisha usalama na ulinzi wa raia na mali zao.”

Vilevile, alisema kituo hicho kitasaidia kupunguza matukio ya uhalifu kwenye makazi na uchomaji moto misitu.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi hao, Diwani wa Igoma, Andrew Mwaipopo, alisema wanahitaji misaada ili kutekeleza miradi mingine ya maendeleo.

Alitaja baadhi ya miradi hiyo kuwa ujenzi wa chuo cha Mamlaka ya Mafunzo na Ufundi Stadi (VETA) ambacho baadhi ya majengo yake yamefikia hatua ya kuezekwa.

Kwa mujibu wa diwani huyo, katika kata hiyo kuna ujenzi wa Kituo cha Afya ambao unaendelea na kwamba miradi yote hiyo ikikamilika itakuwa na msaada mkubwa hao na wengine wa maeneo ya jirani.

# Wananchi waombwa kufichua wahalifu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi Mkoa wa Mbeya limeomba ushirikiano kwa wakazi mkoani hapa wa kuendelea kutoa taarifa ili kudhibiti uhalifu huo kwa kukamata watuhumiwa.

Ombi hilo lilitolewa na Kamanda wake,Benjamin Kuzaga juzi wakati akizungumza na wandishi wa habari kuhusu hali ya usalama katika mkoa huo na mikakati ya kudhibiti matukio hayo kwa mwaka huu wa 2025.

Kuzaga, alisema jeshi hilo kwa mwaka jana lilishirikiana na wananchi hao kudhibiti wahalifu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo na litaendelea kushirikiana nao 2025.

Alisema jeshi hilo lipo wa ajili ya kuhakikisha linalinda usalama wa raia na mali zao, hivyo ili kuhakikisha usalama unaendelea kuwepo ni lazima kudumisha ushirikiano huo.

“Ukiona watu ambao huwafahamu kwenye eneo lako ni vema ukatoa taarifa ili tuwachunguze na kuchukua hatua, lengo letu ni kuhakikisha tunauanza mwaka 2025 kwa amani na tunaumaliza kwa amani,” alisema Kuzaga.

Alisema jeshi hilo limeanzisha utaratibu wa kufanya doria maeneo yote tete kwa lengo la kuhakikisha hayaendelei kuwa na hali hiyo na wananchi kufanye shughuli zao za uzalishaji kwa amani na utulivu.

Alisema kwenye maeneo yote ya miteremko mikali, watahakikisha utaratibu wa magari makubwa na madogo kupita kwa awamu unaendelea ili kupunguza ajali ambazo zimekuwa zikitokea mara kwa mara na kusababisha vifo.

Aliwasisitiza madereva kuendelea kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka kusababisha ajali, lasivyo wataendelea kuwachukulia hatua kali kwa kuwakamata, kuwafikishwa mahakamani na kuwafutia leseni zao.

Alipiga marufuku madereva kuendesha vyombo hivyo bila kuwa na leseni kwa kuwa ni kosa kwa mujibu wa sheria za nchi.

# SMZ yajikita kujenga hospitali za kisasa Unguja, Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), inatarajia kuanza ujenzi wa hospitali za kisasa katika visiwa vya Unguja na Pemba na kutoa huduma bora kwa wananchi.

Mpango huo umetangazwa na Waziri wa Nchi Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Masoud Ali Mohammed wakati wa hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi katika Kituo cha Afya Sebleni visiwani hapa.

Mohammed, alisema kulingana na wakati ulipo sasa ni wajibu wa serikali kujenga majengo ya kisasa ya hospitali zake na kutoa huduma bora kwa jamii.

Aliwataka watendaji wa wizara hiyo kutunza na kuyaenzi majengo hayo ili kudumu kwa muda mrefu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk Mngereza Mzee Miraji, ujenzi wa kituo ukikamilika, kitakuwa na uwezo wa kuhudumia zaidi ya watu 82,288 wa Shehia ya Amani, Nyerere, Sebleni, Kwawazee, Kwamtumwa Jeni na nyingine jirani.

# Wavuvi watangaziwa neema ya jodari

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI visiwani hapa wametakiwa kuvua samaki aina ya jodari maeneo ya bahari kuu ya Hindi ili kutosheleza mahitaji ya hoteli za kitalii nchini na kuinua kipato chao.

Rai hiyo imetolewa na Waziri wa Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Shaaban Ali Othman katika Tamasha la Vumba lililofanyika Maisara mjini hapa.

Othman, alisema wizara hiyo imetangaza fursa hiyo kwa wavuvi hao kwa kuwa kuna wahitaji wengi wa kitoweo hicho ndani na nje ya nchi hususani katika hoteli hizo.

Alizitaja fursa nyingine kuwa ni mpango wa serikali kutengeneza boti kubwa kuwawezesha kuvua samaki hao katika maeneo ya bahari kuu.

Alisema jodari wana soko la uhakika ndani na nje ya nchi na kuwataka wavuvi kujipanga kuvua katika eneo la maji yenye kina kirefu baharini hapo.

**Mkurugenzi wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sued Hemed alisema bahari hiyo kwa Zanzibar na maeneo ya jirani katika ukanda mkuu kuna jodari wengi.**

Mkurugenzi wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sued Hemed alisema bahari hiyo kwa Zanzibar na maeneo ya jirani katika ukanda mkuu kuna jodari wengi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Hamad Bakari, alisema wamejipanga kufikia wavuvi wakubwa na kufahamu mahitaji yao zaidi ya uvuvi katika bahari kuu.

Bakari, alisema wizara hiyo imeanza kuzungumza na wavuvi aina ya boti wanazotaka kutengenezewa zenye uwezo mkubwa wa kufika bahari kuu kufanya uvuvi mkubwa na kubebwa shehena kubwa ya samaki.

Alisema serikali inataka kuona wavuvi wanamiliki vyombo vya kisasa vya kufika katika eneo hilo na kuvua samaki wakubwa zaidi.




Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (wa pili kulia), akiteta jambo na mmoja wa viongozi wa taasisi ya fedha, Naima Said Shaame (wa pili kushoto), muda mfupi kabla ya kuanza kwa matembezi ya kitaifa katika siku ya mazoezi kitaifa yaliyofanyika wilaya ya Wete mkoa wa Kaskazini Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Barabara vijijini kuinua uchumi wa wakulima

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema imejenga barabara za mjini na vijijini kwa asilimia 80 kwa kipindi cha miaka minne na kukuza sekta ya kilimo na wakulima kupiga hatua kiuchumi.

Hayo yalisemwa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Ikulu, Ali Suleiman Ameir wakati akifungua barabara ya Donge hadi Chaani Mkoa wa Kaskazini Unguja.

Ameir, alisema ujenzi huo umetimiza malengo ya serikali kujenga mtandao wa barabara ya kuwainua wakulima kiuchumi.

Alisema kuwapo kwa barabara imara kwenda vijijini, kutaongeza uzalishaji wa mazao kwa wakulima na kufikisha kwenda mjini kipindi cha mvua.

Aliwataka wakulima na wananchi kwa kutumia fursa ya kuwapo kwa barabara hizo za lami kulima mazao mbalimbali na kuyafikisha sokoni.

"Ujenzi wa barabara za kiwango cha lami zinazokwenda vijijini ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) hatua ambayo itawawezesha wakulima na wananchi kurahisisha usafiri kwao na mazao hadi mijini kwenye masoko," alisema Ameir.

Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Dk. Makame Machano, alisema serikali imejipanga kutengeneza mtandao wa barabara katika Kisiwa cha Unguja na Pemba.

Dk. Machano, alisema barabara hizo ni kuu na zile za kwenda vijijini zenye urefu wa kilomita 275 na kuifungua Zanzibar.

Alisema mtandao wa barabara zinazokwenda maeneo huru ya kiuchumi na miradi ya utalii, zimejengwa hivyo kutoa nafuu kwa wananchi na wawekezaji waliopo nchini kuendesha shughuli zao.

"Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi tumefanikiwa kwa kiasi kikubwa kujenga miundombinu ya barabara kwenda vijijini katika mashamba ya wakulima na wawekezaji na kutuongezea fursa za kiuchumi," alisema Dk. Machano.

Baadhi ya wakazi wa Donge na Chaani wamefurahishwa na ujenzi wa barabara hiyo kwenye maeneo yao kwa kuwa itafunguwa fursa nyingi za uchumi miongoni mwao.

# HABARI PICHANI



Waimbaji wa kwaya ya kusifu na kuabudu kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania Usharika wa Mlandege, mjini Iringa, wakiimba nyimbo za kumshukuru Mungu kwa kuvuka mwaka 2024 na kuanza mwaka mpya 2025 wakati wa mkesha kanisani hapo jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**



Mmoja wa waumini akiwa kwenye maombi wakati wa mkesha wa Mwaka Mpya jana. **PICHA: FRANCIS GODWIN**




Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza, mkoani Tanga, Elias Majo (kushoto), akiwatambulisha wageni wake jana katika Ibada ya Mwaka mpya kanisani hapa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Mchungaji wa Kanisa la Anglikana mtaa wa Madaba wilayani Muheza mkoani Tanga, Paul Luhinga, akiwaombea baraka waumini wa kanisa hilo waliyotoa ushuhuda wao wa mwaka uliopita na kuingia mwaka mpya wa 2025 jana katika Ibada ya Mwaka Mpya. **PICHA: STEVEN WILLIAM**



Baadhi ya waumini wakiwa katika ibada maalum ya Adhimisho la Misa Takatifu ya Sherehe ya Bikira Maria Mama wa Mungu na Mwaka Mpya 2025 iliyofanyika katika Kanisa Katoliki Parokia ya Mwenyeheri Maria Theresa Ledochowska Kiwanja cha Ndege Dodoma jana. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



Baadhi ya waumini wakiwa katika ibada ya Adhimisho la Misa Takatifu ya Sherehe ya Bikira Maria Mama wa Mungu na Mwaka Mpya 2025. **PICHA: OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

HABARI KIMATAIFA

# Ivory Coast yaitaka Ufaransa kuwaondoa wanajeshi wake

**YAMOUSSOUKRO, Ivory Coast**

IVORY Coast imetangaza kuondoka rasmi kwa wanajeshi wa Ufaransa katika hilo la Afrika Magharibi, na kupunguza ushawishi wa nchi hiyo kijeshi.

Katika hotuba ya mwisho wa mwaka, Rais wa Ivory Coast, Alassane Ouattara, alisema hatua hiyo ni kielelezo cha kuanza kwa jeshi la kisasa la nchi hiyo.

Nchi jirani ya Senegal, ambayo mwezi uliopita ilitangaza Ufaransa itafunga kambi zake za kijeshi kwenye eneo lake, ilithibitisha kuwa hatua hiyo itakamilika mwishoni mwa 2025.

Ivory Coast ina wanajeshi 600 wa Ufaransa na kuwa na kambi kbwa ya kijeshi ya Ufaransa katika Afrika Magharibi.

Aidha nchini Senegal ina wanajeshi 350.

„Tumeamua kwa njia ya pamoja kuondoa vikosi vya Ufaransa ndani ya Ivory Coast,“ alisema Rais Ouattara.

Aliongeza kuwa kikosi cha wanajeshi cha Port Bouét ambacho kinaendeshwa na jeshi la Ufaransa kitakabidhiwa kwa wanajeshi wa Ivory Coast.

Ufaransa, ambayo utawala wake wa kikoloni huko Afrika Magharibi ulimalizika miaka ya 1960, tayari imewaondoa wanajeshi wake kutoka Mali, Burkina Faso na Niger kufuatia mapinduzi ya kijeshi katika nchi hizo na kuongezeka hisia za chuki dhidi ya taifa hilo.

Serikali ya Chad ambayo ni mshirika mkuu wa katika mapambano dhidi ya wanamgambo wa Kiislamu katika eneo hilo, ilikatiza ghafla mkataba wake wa ushirikiano wa ulinzi na Ufaransa mwezi Novemba.

Rais wa Senegal Bassirou Dioumaye Faye alisema: „Nimemuagiza waziri wa Ulinzi, kupendekeza mafunzo mapya ya ushirikiano katika ulinzi na usalama baada ya kumalizika kwa uwepo wa jeshi la kigeni nchini Senegal kuanzia 2025.“ Alisema kiongozi huyo.

Faye alichaguliwa mwezi Machi kwa ahadi ya kutoa mamlaka na kukomesha utegemezi kwa nchi za kigeni.

Ufaransa itabaki na Gabon katika ushirikiano wa kijeshi.

Viongozi wa kijeshi wa Niger, Mali na Burkina Faso wameelekeza urafiki na Russia tangu walipowatimua wanajeshi wa Ufaransa katika nchi zao.

Russia ilituma mamluki katika eneo la Sahel ili kuwasaidia kupambana na waasi wa kijihadi.

Kuna dalili kwamba Ufaransa sasa imebaki na wanajeshi wasiozidi 2,000 nchini Djibouti na Gabon.

Wachunguzi wa masuala ya kisiasa wanaamini kuwa Ufaransa imekuwa ikifanya juhudi za kufufua ushawishi wake wa kisiasa na kijeshi unaopungua barani Afrika. Koloni hilo la zamani ya kisiasa sasa inaonekana kubuni mkakati mpya wa kijeshi wa kupunguza uhusiano wa kijeshi, hatua ambayo ingepunguza kwa kasi uwepo wake wa kudumu wa askari katika bara hio.

Ivory Coast ilisifiwa kama kielelezo cha utulivu. Lakini uasi wa silaha uliotokea 2002 uligawanya taifa hilo sehemu mbili.

Licha ya kukosekana kwa utulivu, Ivory Coast ndiyo muuzaji mkubwa zaidi wa kakao duniani, na raia wake wanafurahia kiwango cha juu cha mapato ikilinganishwa na nchi nyingine katika eneo hilo.

*BBC*



Wakazi wa Jiji la Bgahdad, Iraq wakifurahia mafataki ya kuukaribisha Mwaka Mpya wa 2025 usiku wa kuamkia jana. **PICHA: AFP**

# Ukraine yafunga mabomba yanayopeleka gesi Ulaya

**KYIV, Ukraine**

UKRAINE imefunga mabomba yanayosafirisha gesi kutoka Russia kupitia ardhi yake hadi nchi za Ulaya tayari.

Hata hivyo, uamuzi huo umeibua matatizo katika eneo la mashariki mwa bara hilo. Taifa la Moldova limetangaza hali ya hatari baada ya kukosa gesi na Slovakia imetishia kulipiza kisasi kwa Ukraine kutokana na kuchukua hiyo.

Chini ya mpango wa miaka mitano uliosainiwa mwaka wa 2019 Ukraine iliiruhusu Russia kusafirisha gesi hadi Ulaya kupitia ardhi yake.

Makubaliano hayo yanamalizika Januari mosi na Ukraine ilisema haina nia ya kurefusha mkataba huo kutokana na uvamizi wa Russia katika ardhi yake.

Mataifa kadhaa ya Ulaya Mashariki bado inategemea gesi kutoka Russia kwa ajili ya kukidhi mahitaji yao ya nishati.

Ilieleza Moldova, ambayo inapakana na Ukraine inakabiliwa na hali mbaya ya ukosefu wa nishati, huku ikipambana na wanaharakati wanaotaka kujitenga ambao wanaungwa mkono na Russia

Nayo Slovakia imetishia kusitisha usambazaji wa umeme nchini Ukraine, hasa baada ya miundombinu ya kuharibiwa vibaya katika mashambulizi ya Russia.

*DW*

## Mayotte kujengwa upya

**PARIS, Ufaransa**

WAZIRI Mkuu wa Ufaransa, François Bayrou anatarajiwa kuzindua mpango kabambe wa ujenzi wa kisiwa cha Mayotte.

Hatua hiyo imefuatia ziara yake kwenye kisiwa hicho katika Bahari ya Hindi wiki tatu zilizopita baada ya Kimbunga Chido kusababisha maafa.

Waziri Mkuu huyo wa Ufaransa alisema rasimu ya sheria ya dharura inayolenga kuijenga upya Mayotte ndani ya miaka miwili itawasilishwa bungeni mwezi Januari.

Ziara ya Bayrou inafuatia ile ya Rais wa Ufaransa Emmanuel Macron, huku baadhi ya wakazi wa Mayotte wakiidai kuwa serikali ya Ufaransa ilikuwa imetelekeza kwa muda mrefu.

*DW*

## FBI yakamata mabomu 150 ndani ya nyumba

**WASHINGTON, Marekani**

SHIRIKA la ujasusi la Marekani FBI, limegundua zaidi ya mabomu 150 yakiwa yamehifadhiwa kwenye shamba moja katika jimbo la Virginia.

Idadi hiyo ya mabomu inaelezwa kuwa ndiyo hifadhi kubwa zaidi ya aina hiyo iliyokamatwa na wakala wa shirika hilo katika historia yake.

Mwanaume mmoja, Brad Spafford alikamatwa Desemba 17 katika kaunti ya Wight County, baada ya mtu mmoja kutoa taarifa kwamba alikuwa akihifadhi silaha na risasi za kujitengenezea nyumbani kwenye makazi anayoishi na mke wake na watoto wawili wadogo.

Wapelelezi hao walisema baadhi ya mabomu hayo yaipatikana katika chumba cha kulala yakiwa ndani ya begi la mgongoni ambalo halina ulinzi lililoandikwa „#nolivesmatter“, alama ambayo inatumiwa na wanachama wa vuguvugu la mrengo wa kulia, linalopinga serikali.

Wakili Spafford alikanusha kuwa mteja wake ni hatari kwa jamii na anataka aachiliwe kutoka kizuizini kabla ya kesi yake kuanza kusikilizwa.

*BBC*

## Wachezaji wamkosha kocha Simba

**Na Faustine Feliciane**

BAADA ya juzi kuibuka na ushindi mnono wa mabao 5-0 dhidi ya Alliance Girls, Kocha wa Simba Queens, Yussif Basigi, amesema anavutiwa na kufurahishwa na uwezo wa wachezaji wake.

Basigi, alisema sababu kubwa ya kupata ushindi kwenye michezo yao ni kujituma kwa wachezaji wake na kufuata maelekezo yake wakiwa mazoezini mpaka kwenye mechi.

Akizungumza na Nipashe juzi, kocha huyo alisema wachezaji wake wanafanya kazi yake iwe rahisi kutokana na namna wanavyopambana na kufuata maelekezo yake.

"Nimeridhishwa na uwezo wa wachezaji wangu, kila mmoja anafanya kazi nzuri na kufanikisha ushindi kwenye michezo yetu, ushindi dhidi ya Alliance Girls umetokana na kujituma kwa wachezaji wake," alisema Basigi.

Alisema anafurahi kumaliza mzunguko wa kwanza akiwa juu ya msimamo huo kwake ni zawadi ya mwaka mpya kwa mashabiki na wapenda soka wa Tanzania.

"Tumemaliza mzunguko wa kwanza tukiwa kileleni, tumecheza michezo tisa na kufanikiwa kushinda nane na kutoka sare mchezo mmoja, hii ni zawadi ya mwaka mpya kwa mashabiki wa Simba," alisema Basigi.

Mchezo wa mwisho mzunguko wa kwanza waliocheza juzi dhidi ya Alliance Girls kwenye uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, Simba ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 5-0.

# MORRISON, KENGOLD WAMALIZANA RASMI

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI usajili kwenye kipindi cha dirisha dogo ukiendelea, Klabu ya KenGold imetangaza kukamilisha dili la kumchukua winga wa zamani wa timu za Simba na Yanga raia wa Ghana, Bernard Morrison, huku winga wa Simba, Salehe Karabaka aliyesajiliwa kutoka JKU, akienda Namungo FC kwa mkopo.

Habari zilizopatikana jana kutoka ndani ya klabu ya KenGold zinasema kuwa imefanikisha kumsajili mchezaji huyo kama mchezaji huru kwa mkataba wa miezi sita ambao utatamatika mwishoni mwa msimu huu.

Awali gazeti hili liliripoti kuwapo kwa mazungumzo ya pande zote mbili huku mchezaji mwenyewe akitaka mshahara wa Sh. milioni 10 ili asaini.

"Kuna vitu vichache tu ambavyo tunakamilisha ili aanze kuitumikia timu, unajua huyu si raia wa Tanzania kwa hiyo kuna mambo ya vibali kwa kufanya kazi na vitu vingine, tukikamilisha tutatangaza rasmi, lakini suala lake limekwisha ila mshahara siwezi kujua ni kiasi gani labda viongozi wa juu wenyewe wanaweza kusema," alisema mtoa taarifa kutoka KenGold.

Morrison aliyejizolea umaarufu mkubwa nchini kutokana na kipaji chake kikubwa cha soka, pamoja na aina yake ya maisha ya kujichanganya na mashabiki, aliingia nchini mwaka 2020 na kujiunga na Yanga akitokea DC Motema Pembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, akaitumikia kwa miezi sita kabla ya kutimkia Simba alipokipiga kwa mwaka mmoja na nusu hadi 2022, aliporejea tena Yanga.

Hata hivyo Yanga hakukaa kwa muda mrefu tena akatimkia AS Rabat ya Morocco ambako alitumikia kwa muda mfupi na kupata majeraha na kumaliza mkataba wa mwaka mmoja akiwa nje ya dimba.

Wakati huo huo, taarifa zingine za usajili zinasema kuwa winga wa Simba, Karabaka amepelekwa kwa mkopo wa miezi sita kwenye klabu ya Namungo.

Taarifa zinasema mchezaji huyo aliomba mwenyewe kuondoka kwenye dirisha hili dogo kwenda timu yoyote ili apate nafasi ya kucheza.

Habari zinasema Namungo wamekubali kulipa mshahara wote wa mchezaji huyo kwa kipindi hicho cha miezi sita ya mkopo na wakati wowote kuanzia leo inaweza kumtangaza rasmi.




Simba Queens imetangaza kumsajili golikipa mpya kutoka Kenya, Wilfrida Cedar, ambaye ataanza kuitumikia timu hiyo kwenye michezo ya Ligi Kuu. **PICHA: SIMBA**

# Mbeya City yasajili wawili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mbeya City inayoshiriki Ligi ya Championship imefanikiwa kupata saini ya nyota wawili, golikipa wa Biashara United, Diey Makonga na mshambuliaji, Kelvin George, Mtanzania aliyekuwa anacheza soka la kulipwa katika klabu ya AS Port ya Djibouti ikiwa ni sehemu ya kukiimarisha kikosi cha timu hiyo.

Taarifa rasmi iliyotolewa jana na klabu hiyo, inasema nyota hao ni baadhi tu ya wachezaji ambao imewasajili kipindi hiki cha usajili wa dirisha dogo.

"Tumefanya usajili wa golikipa kutoka Biashara United, Diey Makonga, ili kuongeza nguvu kwenye eneo la ulinzi, lakini pia tumemsajili mshambuliaji kijana wa Kitanzania akitokea klabu ya AS Port ya Djibouti, akiwa amepitia klabu mbalimbali hapa nchini," ilisema taarifa hiyo.

Mbeya City imepanda hadi nafasi ya pili katika msimamo wa Ligi ya Championship, baada ya juzi kuichapa Cosmopolitan bao 1-0 kwenye Uwanja wa Mabatini, Pwani na kufikisha pointi 31 pointi nne nyuma ya Mtibwa Sugar iliyo kileleni.

Klabu hiyo imesema bado inaendelea kuangalia ni sehemu gani zenye mapungufu ili kuleta maingizo mapya lengo likiwa kupambana kurejea Ligi Kuu msimu ujao.

Timu hiyo ilishuka daraja msimu wa 2022/23 baada ya kufanikiwa kupanda na kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu wa 2013/14 na kuwa moja kati ya timu tishio.

Wakati huo huo, Ligi ya Championship iliendelea juzi kwenye viwanja mbalimbali, ambapo Kiluvya FC iliichapa African Sports bao 1-0, Bigman FC ikiwa nyumbani ilitoka suluhu na Mbuni FC.

Matokeo ya mechi hizo yanaifanya Kiluvya kufikisha pointi saba ikiwa nafasi ya 15, African Sports nafasi ya 12 kwa pointi zake nane, Mbuni nafasi ya nane ikiwa na pointi 20 na Bigman nafasi ya tisa ikiwa na pointi 19.

## ZISIKUPITE

### LIVERPOOL IMEIGOMEA MADRID
LIVERPOOL imekataa mpango wa Real Madrid wa kutaka kumsajili beki wa kulia wa England, Trent Alexander-Arnold mwenye umri wa miaka 26 mwezi huu. ***(Athletic)***

### ZIRKZEE AWANIWA SERIE A
JUVENTUS na Napoli ZA Serie A zinania ya kumsajili mshambuliaji wa Manchester United na Uholanzi, Joshua Zirkzee mwenye umri wa miaka 23. ***(Mirror)***

### MAN HAINA BAJETI USAJILI
KLABU ya Manchester United haina bajeti ya kuimarisha kikosi chao mwezi huu na watalazimika kuuza wachezaji kwanza kabla ya kununua ili kuwa na faida na kuendana na sheria za uchezaji wa haki za Kifedha endelevu. ***(Manchester Evening News)***

### SALAH, VAN DJIK KUONGEZA
WINGA wa Misri, Mohamed Salah mwenye umri wa miaka 32 na mlinzi wa Uholanzi Virgil van Dijk mwenye miaka 33, wote wanatarajiwa kuongeza muda wao wa kukaa Liverpool kwa miaka miwili zaidi. ***(David Ornstein, via Mirror)***

### LIVERPOOL KUMPIGA BEI NUNEZ
LIVERPOOL ipo tayari kumuuza mshambuliaji wa Uruguay, Darwin Nunez mwenye umri wa miaka 25 na wamemuona mshambuliaji wa Inter Milan na Ufaransa, Marcus Thuram mwenye umri wa miaka 27 pamoja na mshambuliaji wa Newcastle United na Sweden, Alexander Isak mwenye miaka 25, kama wachezaji wanaoweza kuchukua nafasi yake. ***(Teamtalk)***

### KERKEZ KWENYE RADA ZA UNITED
LIVERPOOL inaweza kushindana na Manchester United katika dili la kumsajili beki wa kushoto wa Hungary, Milos Kerkez mwenye umri wa miaka 21 kutoka Bournemouth. ***(Caught Offside)***

### DANI OLMO AGOMBEWA EPL
ARSENAL, Liverpool, Chelsea na Tottenham zimeungana na Manchester United na Manchester City katika kuwania kumnunua mshambuliaji wa Barcelona mwenye umri wa miaka 26, Dani Olmo. ***(Mundo Deportivo)***

### MADRID YAVUTIWA NA HUIJSEN
REAL Madrid inavutiwa na mlinzi wa Bournemouth na Hispania, Dean Huijsen mwenye umri wa miaka 19. ***(Fichajes)***


### CESARE CASADEI KUTUA TORINO
CHELSEA iko tayari kumuuza kiungo wa kati wa Italia, Cesare Casadei mwenye umri wa miaka 21 ambaye ameivutia klabu ya Torino ya Italia. ***(Talksport)***

### AINA KUPEWA MKATABA MPYA
KLABU ya Nottingham Forest ina uhakika wa kukubaliana mkataba mpya na beki wa pembeni wa Nigeria, Ola Aina mwenye umri wa miaka 28 ambaye pia anafuatiliwa na Manchester City. ***(Football Insider)***

### NKUNKU MBADALA WA OLMO
KLABU ya Barcelona inaweza kumnunua kwa mkopo mshambuliaji wa Chelsea, Christopher Nkunku mwenye umri wa miaka 27 kama watashindwa kumsajili Dani Olmo kwa kipindi cha pili cha msimu. ***(Offside)***

### BAYERN MUNICH KUMSAJILI BART
KLABU ya Bayern Munich imeorodhesha makipa kadhaa ambao wanaweza kuwasajili msimu wa majira ya joto akiwamo nyota wa kimataifa wa Uholanzi mwenye miaka 22, Bart Verbruggen wa Brighton. ***(Bild)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# CASEMIRO KUONDOKA MANCHESTER UNITED

Mbrazil huyo yupo tayari kukaribisha uhamisho wa kuondoka baada ya....

**MANCHESTER, England**

KIUNGO wa kati wa Manchester United, Casemiro atakaribisha uhamisho wa kwenda Ligi Kuu ya Saudi Arabia wakati wa dirisha la uhamisho wa Januari hii, ripoti imedai.

Casemiro mara nyingi amekuwa akihusishwa kuondoka Old Trafford mwaka uliopita.

Uchezaji wake pale United umeonekana kuwa tofauti, huku kiwango chake kikionekana kutokuwa cha kuridhisha.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32, alianza katika kichapo cha Jumatatu dhidi ya Newcastle United, lakini hiyo ilikuwa ni mara ya kwanza kuanza ndani ya mwezi mmoja, baada ya kuwa mchezaji mbadala ambaye hajatumiwa chini ya Kocha Ruben Amorim.

Gazeti la UOL la Brazil limeripoti kwamba hali ya Casemiro pale United „itaharakisha mchakato" na kwamba hakuna „vikwazo vikubwa" ambavyo vinaweza kuzuia kuondoka.

Bado haijajulikana ni klabu gani huko Saudi Arabia anaweza kujiunga nayo.

Mfuko wa Uwekezaji wa Umma (PIF) unamiliki klabu za Al Hilal, Al Nassr, Al Ittihad na Al Ahli na italazimika kuamua mahali pa kumweka Casemiro.

Al Ettifaq inayonolewa na kocha Steven Gerrard inamilikiwa na Wizara ya Michezo ya serikali, wakati Al Qadsiah ni ya Kampuni ya Mafuta ya Saudi Arabia inayomilikiwa na serikali.

Kila klabu kwa sasa iko katika idadi ya juu zaidi ya wachezaji wa nje wanaoruhusiwa, ambayo ina maana kwamba kuondoka kutahitajika ili kuwezesha wapya wanaowasili kutoka nje ya nchi.

Al Nassr inaweza kuwa chaguo la wazi zaidi kutokana na uhusiano wa Casemiro na mchezaji mwenzake wa zamani wa Real Madrid, Cristiano Ronaldo.

Casemiro ni miongoni mwa wachezaji wanaolipwa fedha nyingi zaidi pale Manchester United, pamoja na Marcus Rashford.

# Rooney hana bahati na ukocha

**LONDON, England**



WAYNE Rooney ameondoka kama kocha wa timu ya Plymouth Argyle inayoshiriki Championship kwa kukubali kuachana na klabu hiyo baada ya michezo 25 pekee.

Rooney ambaye ni gwiji wa Manchester United na timu ya taifa ya England, hiyo ilikuwa kazi yake ya nne kama kocha, lakini ameondoka baada ya miezi saba katika klabu hiyo ya Championship huku akiwa ameshinda mechi tano pekee.

"Plymouth Argyle inaweza kuthibitisha kwamba klabu na Kocha Mkuu Wayne Rooney wamekubaliana kuachana mara moja," ilisema taarifa ya Plymouth.

Habari hizi zinafuatia nyakati za kukatisha tamaa kwa Rooney kule Derby County, D.C. United na Birmingham City, ambazo zilishushwa daraja kwenye League One.

Plymouth baada ya kumaliza nafasi juu ya Birmingham mwaka jana, sasa itakuwa na matumaini ya kupambana kupanda daraja.

# Liverpool yaikatalia Madrid kwa Alexander-Arnold

**LIVERPOOL, England**



LIVERPOOL iamekataa mpango wa Real Madrid kutaka kumsajili beki wake wa pembeni Trent Alexander-Arnold katika dirisha la uhamisho la Januari kwa mujibu wa ESPN.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England mkataba wake unamalizika Anfield Juni, na vyanzo vimeiambia ESPN kwamba yeye ndiye mlengwa mkuu wa safu ya ulinzi ya Madrid kutokana na jeraha la muda mrefu la beki wa kulia, Dani Carvajal.

Ilifikiriwa miamba hao wa Hispania walipendelea kusubiri hadi msimu ujao wa majira ya joto ili kumsajili Alexander-Arnold kwa uhamisho wa bure, lakini waliwasiliana na Liverpool Jumanne kuhusu uwezekano wa kumsajili mwezi huu.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba mapendekezo hayo yalikataliwa haraka na vinara hao wa Ligi Kuu na hakuna ofa rasmi iliyotolewa.

Mazungumzo kuhusu kuongezewa mkataba katika klabu ya Liverpool yamekuwa yakifanyika na kambi ya Alexander-Arnold kwa miezi kadhaa, na mchezaji huyo bado hajaonesha nia ya kuondoka katika klabu hiyo.

Alexander-Arnold ni mmoja wa wachezaji watatu wa Liverpool ambao mikataba yao inaisha mwishoni mwa msimu huu, pamoja na mshambuliaji nyota Mohamed Salah na nahodha wa klabu Virgil van Dijk.

Wachezaji wote watatu walio nje ya mkataba wataweza kuongea rasmi na klabu nyingine kuhusu kujiunga nao majira ya joto.

Kikosi cha Arne Slot kiko mbele kwa pointi nane kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu England na pia wameshinda michezo yao yote katika Ligi ya Mabingwa Ulaya iliyoboreshwa, pia wamefanikiwa kutinga nusu fainali ya Kombe la Carabao.



# ARTETA: ARSENAL HAIPOI MBIO ZA EPL

**LONDON, England**

MIKEL Arteta amesema Arsenal lazima "wawe kama nyundo" ili kuwawinda Liverpool katika mbio za kuwania taji la Ligi Kuu England.

Arsenal jana ilicheza na Brentford ikilenga kusonga mbele ya Nottingham Forest inayoshika nafasi ya pili kwa ushindi ambao utawafanya kufikisha pointi sita dhidi ya vinara Liverpool.

Kikosi hicho cha Liverpool kinachoongozwa na Arne Slot kimepoteza mchezo mmoja pekee wa ligi msimu huu na alipoulizwa ni kwa kiasi gani kitakuwa kigumu kukikimbiza, Arteta alisema: "Sijui na haitegemei sisi.

"Tunapaswa kuendelea kuwa kama nyundo, kuwepo kila siku, kila siku na kama mtu kushinda mechi zote basi hongera yake na kwenda kwa msimu ujao."

Jeraha la msuli la Bukayo Saka ambalo linatarajiwa kumweka nje hadi Machi kufuatia upasuaji limetoa fursa kwa Leandro Trossard kupata nafasi ya kucheza.

"Ni tabia nzuri sana," alisema Arteta kuhusu mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji ambaye ameanza mechi 11 pekee msimu huu.

"Wote wanataka kucheza, wanataka kucheza kila wakati.

"Wameonesha uthabiti zaidi katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, anastahili hivyo, amekuwa na ushindani mkubwa kwenye nafasi yake, hivyo hivyo, amepandisha kiwango, akicheza kwa kiwango hicho basi atacheza kama mtu mwingine yeyote..

"Leo kwa kawaida ni mtu wa kupenda kucheza, lakini napenda hivyo kwa sababu ana ushindani mkubwa na ana vipindi vya mazoezi, huwa anashughulika na maamuzi, kwa sababu anataka kushinda. Hicho ndicho ninachopenda.

"Siku zote anataka kuwa bora na asipokuwapo hana furaha. Lakini hiyo ndiyo inamsukuma.

Hapo ndipo anapoingia uwanjani, anaweza kuleta mchango."

# NZENGELI, AUCHO WAMTAJA FEITOTO

**Na Faustine Feliciane**

NYOTA wa klabu ya Yanga, Max Nzengeli na Khalidy Aucho kwa nyakati tofauti wamesema kwa wachezaji wazawa hapa nchini, kiungo wa Azam FC na timu ya taifa 'Taifa Stars', Feisal Salum 'Feitoto' ni mmoja wa wachezaji wenye kipaji na uwezo mkubwa.

Akizungumza jijini Dar es Salaam, Nzengeli alisema kwa wachezaji wa ndani, Feitoto ni mchezaji anayejua mpira na ana uwezo mkubwa.

„Anaweza kucheza popote, ni mchezaji mzuri sana, nadhani watanzania wanatakiwa kujivunia kuwa naye ingawa wapo wachezaji wengine wengi wenye uwezo," alisema Nzengeli ambaye hivi karibuni mchezaji wa Simba, Ladack Chasambi alinukuliwa akimtaja kama mchezaji 'kioo' kwake hapa nchini.

Aidha, mbali na Feitoto, Nzengeli pia amemtaja kiungo wa Simba, Awesu Awesu kuwa ni miongoni mwa wachezaji wenye uwezo mkubwa.

Kwa upande wake, Aucho, mchezaji wa kimataifa wa Uganda, naye alisema pamoja na Tanzania kuwa na wachezaji wengi wenye vipaji na uwezo mkubwa, kwake Feitoto anakaa juu yao.

„Ana uwezo mkubwa sana miongoni wa wachezaji wa Tanzania, huwa namfuatilia akicheza kwenye timu yake ya Azam FC," alisema Aucho.

Kabla ya kujiunga na Azam FC msimu uliopita, Feitoto alikuwa akiichezea Yanga waliomsajili kutoka Singida United wakati ikishiriki Ligi Kuu Tanzania Bara kabla ya kushuka daraja.




Wachezaji wa mpira wa kikapu kwa watu wenye ulemavu, wakifanya mazoezi katika Kituo cha Michezo Jakaya Kikwete, Dar es Salaam kama walivyokutwa juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Yanga SC yaifuata Simba kwa Rupia

INATOKA UK. 24

"Hawa wengine tukiwapata sawa, lakini tukiwakosa pia hakuna tatizo kwa sababu dirisha hili ni gumu, unatakiwa umchukue mchezaji ambao anacheza kwenye timu yake, kwa hiyo wakati mwingine ni ngumu sana klabu kukubali kuwaachia," alisema.

**Wakati huo huo kuelekea kwenye mchezo wa Ligi ya Mabingwa Afrika, kikosi cha TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo, kinatarajiwa kuwasili nchini leo saa 11:00 jioni kwa ajili ya mchezo wa raundi ya nne hatua ya makundi unaotarajiwa kupigwa Jumamosi, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, saa 10:00 jioni.**

Kamwe amesema maandalizi ya mchezo huo yanaendelea chini ya Kocha Mkuu, Sead Ramovic ambaye ameonekana kukibadilisha kikosi hicho kwa muda mfupi.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa, Desemba 4 mwaka jana, kwenye Uwanja wa Mazembe, Lubumbasi, timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1.

Yanga ambao wapo Kundi A, wanahitaji ushindi kwa udi na uvumba kwani ina pointi moja tu mpaka sasa katika michezo mitatu iliyocheza, huku ikiwa inaburuza mkia kwenye msimamo wa kundi hilo.

# Pamba Jiji yajipanga kurudi kivingine mzunguko wa pili

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Pamba Jiji imesema kuelekea mzunguko wa pili wa Ligi Kuu, inaendelea kujipanga na kufanya usajili wa uhakika ili kurejea na makali kwenye mzunguko wa pili wa Ligi Kuu.

Meneja wa timu hiyo, Ezekiel Ntibikeha, alisema mbali na wachezaji iliyowasajili ambao tayari wameshaanza kuonekana kwenye baadhi ya michezo, wanaendelea na usajili mkubwa wa wachezaji ambao watakibadilisha kikosi chao kuwa imara.

„Tulitegemea walau mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu tuwe na pointi 20, lakini tumemaliza na pointi 12, tumeanza na tunaendelea kufanya maboresho makubwa kwa sababu tumeiona ligi ilivyo inahitaji watu wa aina gani, mpaka kufungwa kwa dirisha dogo tutakuwa tayari tumeshamaliza kujaza mapengo maeneo ambayo tunahisi yalihitaji marekebisho," alisema meneja huyo.

Aidha, aliwataka mashabiki wa soka jijini Mwanza kutokata tamaa, badala yake kuiunga mkono timu hiyo ili itimize lengo lake kuu kwa msimu huu ambalo ni kubaki Ligi Kuu.

„Mashabiki wa Mwanza wanatakiwa kutuunga mkono, sisi tutahakikisha tunasajili wachezaji mahiri ambao wanaweza kuitoa timu hapa ilipo na kuipeleka sehemu nyingine, na niziambie tu timu zingine zisikariri, zisitarajie kukutana na Pamba hii ya mzunguko wa kwanza, badala yake watakutana na nyingine kabisa ambayo imeboreshwa," alisema.

Tayari kutoka timu hiyo inaeleza mpaka sasa imeshawasajili Zabona Mayombya kutoka Prisons, Cherif Ibrahim beki wa kushoto kutoka Coton Sport ya Cameroon, Hamad Majimengi, Habib Kyombo, Deus Kaseke, pamoja na kipa Mohamed Kamara raia na Sierra Leone, ambaye ametua kwenye kikosi hicho kwa mkopo akitokea Singida Black Stars.

Timu hiyo ambayo mpaka sasa imecheza michezo 16, ipo kwenye nafasi ya 14 kwenye msimamo wa ligi ikiwa na pointi 12.

Michezo
Alhamisi Januari 2, 2025
Nipashe

## Casemiro kuondoka Man United

UKURASA 21



# YANGA SC YAIFUATA SIMBA KWA RUPIA

●●●Yatangaza kumwania mshambuliaji huyo na mazungumzo yame...

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Yanga imetangaza kuwa inaelekea kukamilisha usajili mmoja mkubwa ambao inatarajia kuutangaza hivi karibuni na kushtua nchi, huku taarifa zikisema imeingilia kati dili la Simba la kumwania straika anayeongoza kwa mabao mpaka sasa kwenye Ligi Kuu, Elvis Rupia.

Awali Simba ilitajwa kuwa kwenye mchakato wa kumsajili mshambuliaji huyo raia wa Kenya na tayari mazungumzo yalishaanza baina ya pande hizo.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Ali Kamwe, alisema kipindi hiki cha dirisha dogo Yanga inafanya usajili wa kuboresha kikosi chake na wanamalizia vitu vichache tu ili kuweza kumtangaza mmoja wa wachezaji ambaye atakuwa gumzo kwenye usajili kipindi hiki.

Hata hivyo, habari kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kuwa ilikuwa kwenye harakati za mwisho kupata saini ya Rupia na ndio wanatarajia kumtangaza wakati wowote kuanzia sasa akitokea Singida Black Stars.

"Katika dirisha hili dogo la usajili tumeshafanya usajili wa kwanza kwa kumsajili Israel Mwenda kwa mkopo hadi mwisho wa msimu akitokea Singida Black Stars, kwa mujibu wa Ofisa Mtendaji Mkuu wetu Andre Ntine alinidokeza kuwa wapo wachezaji wengine ambao wataongezwa kwenye kikosi chetu, katika mapendekezo ambayo yametolewa, siku hizi mbili tutakwenda kukamilisha moja ya sajili kubwa sana.

Nimeshuhudia mchakato wake ulivyokuwa wa kusumbuana sana, lakini hatimaye uongozi umeweza kukamilisha dili hilo, kila kitu kimekwenda vizuri bado vitu vichache sana tutakuja kumtambulisha. Uzuri ni kwamba usajili huu hauna mbwembwe sana, ukipata mtu anatakiwa kutambulishwa mapema, watu watashangaa sana na wengine tutawaliza," alisema Kamwe.

Alisema mbali na huyo, wapo wengine ambao uongozi unaendelea na mazungumzo ingawa kumekuwa na ugumu kupata wachezaji kipindi hiki.

INAENDELEA UK. 23



Rupia

## Fadlu: Tutapambana uwanjani dakika zote

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI kikosi cha Simba kikitua salama nchini Tunisia tayari kwa mchezo wao wa marudiano wa Kombe la Shirikisho hatua ya makundi dhidi ya CS Sfaxien, Kocha wa timu hiyo, Fadlu Davids amesema wapo tayari kwa mchezo huo na wachezaji wake watapambana dakika zote.

Simba Jumapili itacheza mchezo huo muhimu ugenini kujaribu kusaka pointi tatu zitakazowaweka kwenye mazingira mazuri ya kufuzu hatua ya robo fainali ya michuano hiyo.

Akizungumza muda mfupi baada ya kutua nchini humo, Fadlu, alisema hawana cha kuhofia katika mchezo huo kikubwa wanapaswa kucheza kwa malengo waliyojiwekea kuweza kupata ushindi.

"Nafahamu hautakuwa mchezo mwepesi, lakini lazima tupambane kuhakikisha tunapata ushindi, wapinzani wetu najua wamejipanga kujaribu kulipa kisasi kwa kufungwa mchezo wa kwanza, lakini tumejiandaa kuwakabili," alisema Fadlu.

Aidha, alisema pamoja na kuhitaji ushindi, watacheza kwa tahadhari mchezo huo na kuwa na nidhamu ya ulinzi huku wakipanga mashambulizi yao vizuri.

Katika hatua nyingine, Meneja Habari wa klabu hiyo, Ahmed Ally, alisema kikosi cha timu hiyo kimetua salama nchini humo huku kila mchezaji akiwa na morali na mchezo huo.

"Wanasimba waliobakia nyumbani waiombee timu yao kuweza kupata ushindi, ni mchezo mzuri na kila mchezaji anafahamu umuhimu wake, tumekuja kuwashangaza waarabu nyumbani kwao," alisema Ahmed.

Alisema katika mazungumzo yake na wachezaji wa timu hiyo, kila mmoja ameonyesha kuwa na shauku na kuitamani mechi hiyo ya Jumapili.

"Wachezaji wana morali sana, kila mmoja mawazo yapo kwenye mchezo huu, wanafahamu umuhimu wa ushindi, mchezo huu ni muhimu sana kwetu kwenye harakati za kuingia robo fainali, matokeo tutakayoyapata hapa yatatupa taswira kamili ya safari yetu kuelekea robo fainali," alisema Ahmed.

Kwenye kundi lao Simba ina pointi sita sawa na Bravo do maquiz ya Angola, CS Costantine huku Cs Sfaxien wakiwa hawana pointi.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >